epaper.ippmedia.com
MIAKA 30 Nipashe
Mwanga wa Jamii
www.ippmedia.com

# Nipashe

Jumanne Februari 4, 2025 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581942

www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII

Nipashe digital 0677 020 710 nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ LIKE & FOLLOW US

UKURASA WA 4

**Neema** yaishukia shule iliyojengwa jirani na makaburi

UKURASA WA 5

**Injini** za Airbus zaitia hasara ya bil. 127/- ATCL kila mwaka



UKURASA WA 5

**Miaka** 48 ya CCM kutumika kufanikisha mkakati maalum kwa wagombea wa urais

**MARTINEZ AZUSHA HOFU MAN UNITED** UK. 22

# Vifurushi NHIF vyapokewa kwa hisia tofauti

UKURASA 3



Mkurugenzi Mkuu wa NHIF, Dk. Irene Isaka



Rais Samia Suluhu Hassan akiteta jambo na Jaji Mkuu, Prof. Ibrahim Juma, wakati wa maadhimisho ya Siku ya Sheria kitaifa, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Samia awaonya majaji, mahakimu kujifanya miungu watu utoaji haki

UKURASA 2

## MAKALI YA TRUMP

# Wadau wataja athari za miradi ya afya kusitishwa

UKURASA 2



**MICHEZO** RAMOVIC AFUNGUKA MAZITO YA MWENDA UK.24

**MAONI,** UK.6

HABARI KITAIFA

# Samia aonya majaji, mahakimu kujifanya miungu utoaji haki

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

RAIS Samia Suluhu Hassan, amewataka majaji na mahakimu nchini, kuacha kuwa miungu watu katika utoaji wa hukumu na kuwataka watende haki kwa misingi ya sheria na Katiba ya nchi.

Pia, amewasihi wakati huu wanapoanza mwaka mpya wa mahakama, wazikague nafsi zao na dhamira kwa kudhamiria daima kukaa kwenye upande wa haki.

Rais Samia, alisema hayo jana jijini hapa, wakati akifunga maadhimisho ya Siku ya Sheria Tanzania, yaliyofanyika kwenye viwanja vya Chinangali.

"Niwakumbushe mwaka 1984 Mwalimu Julius Nyerere akihutubia kwenye mkutano wa majaji na makimu, aliwaasa watumishi kwa wakati huo kwa kuwaambia kwamba jaji au hakimu ni dhamana ambayo inataka uadilifu na nidhamu yako isitiliwe shaka hata kidogo hiyo ndio sifa ya kuwa jaji au hakimu.

"Nami niungane na kauli hiyo na niseme kwamba kazi ya kutoa haki ni kazi ya Mwenyezi Mungu, ambaye mbali na utoaji haki yeye ana jaala na kudra ambavyo pia huvitumia kumkadiria mwanadamu," alisema Rais Samia.

Aidha, alisema majaji na mahakimu ni mawakala wa utoaji haki duniani, lakini wamenyimwa jaala na kudra na kwamba wanapaswa kufanya kazi zao kwa kufuata makubaliano ya Katiba na Sheria za nchi kama zilivyowekwa.

"Niwasihi sana, niwaombe sana tusiwe mungu watu hatuna sifa ya kudra wala jaala tutoe haki kwa misingi ile ambayo tumekubaliana na tumeiweka kisheria na kikatiba, niwasihi mnavyo anza mwaka mpya wa mahakama kagueni nafsi zenu na dhamira zenu daima chagua kukaa upande wa haki," alisisitiza Rais Samia.

Aidha, alisema kutokana na kazi nzuri iliyofanyika hivi sasa kwenye haki jinai ipo haja ya kuweka nguvu kwenye upande wa haki madai.

Alisema kuwekeza nguvu kwenye haki madai kutasaidia serikali kutekeleza kwa ufanisi Dira ya Maendeeo ya Taifa ya Mwaka 2050.

Alisema ili kufanyika hilo mahakama pamoja na wadau wengine wanapaswa kujipanga kwenye utekelezaji wa dira hiyo.

Pia, alisema kutokana na uwekezaji kwenye haki jinai kwa mwaka 2024, jumla ya mashauri 172,301 yalisajiliwa na kumalizika kwa kutumia mfumo wa mtandao katika ngazi ya Mahakama za Mwanzo.

"Aidha, jumla ya mashauri 17,714 yalisikilizwa na kumalizika kwa njia ya mtandao katika mahakama za wilaya hadi mahakama kuu ambapo baadhi ya wadaiwa na mashahidi walitoa ushahidi wao kwa njia ya mtandao jambo ambalo hapo zamani ilikuwa kama ndoto," alisema.

Jaji Mkuu wa Tanzania, Profesa Ibrahim Juma, alisema migogoro ya ardhi imekuwa ni sehemu kuu inayozalisha mashauri ya jinai nchini.

Alisema kama eneo la ardhi litawekwa sawa litasaidia kupunguza mashauri ya jinai nchini, lakini pia kuipunguzia mzigo mahakama nchini.

Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Hamza Johari, alisema watafanya marekebisho ya sheria zote ambazo haziendani na Dira ya Maendeleo ya Taifa ya mwaka 2050 ili zikidhi mahitaji ya sasa.

Hamza alisema ili Dira ya Maendeleo ya Taifa ya 2050, ifanikiwe ipo haja ya kuboreshwa kwa sheria ili ziendane na kasi ya dira hiyo.

"Ili kufikia malengo ya Dira ya Maendeleo ya Taifa ya 2050 ipo haja kufanyika kwa maboresho ya sheria ili zikidhi matakwa na dira badala ya kukidhana," alisema Hamza.

Kadhalika, alisema katika kipindi cha kuanzia Julai hadi Desemba, mwaka jana, Sheria Kuu 300, zimefanyiwa tafsiri kutoka lugha ya Kingereza kwenda Kiswahili.

Naye Rais wa Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS), Wakili Boniface Mwabukusi alisema chama hicho kitaendelea kujenga na kuimarisha ushirikiano na serikali, na kwa kufanya hivyo hawajalamba asali.

Mwambukusi, pia alisema wanaposhirikiana na serikali haimaanishi wamepewa rushwa ama pesa ili kuwafunga midomo.

Hata hivyo, alisema TLS sio kikundi cha magaidi bali ni 'Statutory body' (chombo cha sheria), katika sehemu za kuonya kitaonya na kupongeza kitapongeza kwa haki na kama kushiriki kazi za nchi kitashiriki pamoja ili kulijenga taifa na kumhudumia Mtanzania.


**KAMPUNI YA MIZIZI AFRICAN COMPANY LIMITED INAYOPATIKANA MUYUNI "A" KIZIMKAZI YENYE NO YA USAJILI Z0000122546, SLP 1994, MKOA WA KUSINI ZANZIBAR**

**KAMPUNI AMBAYO INA WAMILIKI WAFUATAO:**

- **REBECCA DU PLESSIS**
- **GREGOR GUENTHER**

MNATANGAZIWA KUWA MNATAKIWA KUFIKA MAHAKAMA KUU YA TUNGUU KWENYE CASE YA GUENTHER VEIT VS MIZIZI AFRICAN COMPANY KESI NAMBA 62/2024 SIKU YA TAREHE 05/02/2025 MBELE YA MUHESHIMIWA SALMA HASSAN KATIKA MAHAKAMA KUU TUNGUU.

NB: KUSHINDWA KUFIKA MAHAKAMANI SIKU YA TAREHE 05/02/2025, MAHAKAMA KUU YA TUNGUU MBELE YA MUHESHIMIWA SALMA HASSAN ITASIKILIZA SHAURI (KESI) HIYO KWA UPANDE MMOJA (EXPRTE HEARING)


# Wadau wataja athari miradi ya afya kusitishwa

**Na Christina Mwakangale**

WADAU wa afya nchini wametaja makundi yatakayoathirika na uamuzi wa kusitishwa ufadhili wa miradi ya afya, ukiwamo wa Mpango wa Dharura wa Rais wa Marekani wa kukabiliana na Ukimwi (PEPFAR), ni wanaoishi na maambukizi ya Virusi Vya Ukimwi.

Wengine ni waraibu wa dawa za kulevya pamoja na kudorora kwa uchumi wa sekta binafsi, kutokana na kundi kubwa kuajiriwa na taasisi na asasi zilizotegemea misaada hiyo.

Akizungumza na gazeti hili, Mkurugenzi wa Kituo cha Life and Hope Sober House (LHRO), Al-Karim Bhanji, amesema tangu Oktoba, 2024, walianza kutekeleza kuwaibua waraibu wa dawa za kulevya, kuwapeleka kliniki za methadone, kupima VVU, Kifua Kikuu (TB) na kuanza dawa, mradi ambao ungekamilika Septemba, mwaka huu.

"Sisi LHRO, kwa mradi tulioyoitekeleza upande wa Dar es Salaam, tuliyofanya na MDH na Bagamoyo THPS imetuathiri, kwa sababu tulikuwa katika mkataba mpya ambao ulianza mwezi wa 10, 2024.

"Kusitishiwa ina maana wafanyakazi wote pamoja na mimi mwenyewe mkurugenzi. Unakuta hatuwezi kwenda kuibua waraibu wapya kwenye maskani, ili tuwapeleke katika kliniki za 'methadone'.

Alisema hatua hiyo imekuja ghafla kabla ya taasisi hizo kujiandaa na kwamba ipo haja ya uamuzi kama huo kufikiriwa mara mbili hasa mfadhili ambaye ni Marekani, pamoja na serikali za nchi husika.

"Kuna wenzetu ambao wanakunywa dawa za ARVs, hatujui hatima itakuwaje, ijapokuwa wamesema watatoa nafuu. Vilevile tunaamshwa kwamba kuwa na mpango B kuwa na vyanzo vya mapato kwa masuala haya, ili kupata ufadhili kutoka ndani, tukopeshwe, tuendelee na kazi tuliyoianza," alisema.

Paul Makuri, mdau wa afya, alisema eneo la huduma za afya mfadhili mkubwa ni PEPFAR, kwa ajili ya VVU, TB na Malaria katika utoaji wa dawa, huduma za upimaji na ufuatiliaji wa wagonjwa pamoja na kufanyika utafiti.

"Akisimamisha msaada huduma zitasimama hasa za kitaalamu, ili watu wafikiwe, sasa zitapatikana huduma kwa gharama kubwa, ambazo wengi hawatamudu.

"Ajira pia zitaathirika kutokana na wengi wamejiriwa kutoa huduma kwenye hii miradi, kama vile wauguzi, wataalamu wa afya na wamekuwa wakilipwa mishahara kupitia hiyo miradi.

"Watu wenye VVU wako milioni 1.5 nchini, wanahudumiwa na kupatiwa dawa. Pia kuna watu wameajiriwa kutafuta ambao wanapotea katika orodha ya kutumia dawa, wanawafuatilia kujua wako wapi, wanaendeleaje. Hata waliokuwa kwenye dawa wanajulishwa, wanaowajulisha watashindwa kufanya kazi," alieleza.

Aliongeza kwamba watoa huduma za Kituo cha Udhibiti wa Magonjwa (CDC), wameathiriwa pia kutokana na kusimamishwa kwa sababu fedha zilizotegemewa kutoka Marekani.

Neema Khalid kutoka Shirika la Wanawake Wanaoishi na Maambukizi ya Virusi vya Ukimwi Tanzania (DWWT), alisema kuzuia utoaji wa fedha kwa eneo la VVU na TB kunaathari kwa nchi na watu, hasa katika nchi zinazoendelea ambazo hutegemea msaada wa kimataifa kwa huduma za afya.

"Baadhi ya athari kuu ni kupungua kwa huduma za afya, vituo vya afya kupungukiwa na rasilimali za msingi, kama dawa za kufubaza makali ya virusi vya UKIMWI (ARVs), matibabu ya kifua kikuu (TB), vipimo na vifaa vya kinga.

"Wagonjwa wanaweza kukosa huduma za mara kwa mara, na hii inaweza kusababisha kuzorota kwa hali zao za kiafya; kuongezeka kwa vifo; kukosekana kwa dawa na huduma za kuzuia maambukizi mapya kunaweza kusababisha vifo vya watu wanaoishi na HIV au TB, hasa wale walioko katika hatua za mwisho za ugonjwa.

"Kuvurugika kwa programu za kuzuia VVU na TB hutegemea ufadhili wa nje. Kuzuia fedha kutasababisha programu hizi kusimama na hii inaweza kuvunja maendeleo yaliyofikiwa katika miaka iliyopita.

"Kwa ujumla, hatua kama hii inaweza kurudisha nyuma mafanikio makubwa yaliyopatikana katika kupambana na HIV na TB na kusababisha madhara makubwa kwa watu."

**TAMKO RASMI**

Tamko rasmi la kusitishwa kwa shughuli zote zilizo chini ya PEPFAR/CDC katika miradi ya Afya Hatua, lilitolewa mwishoni mwa wiki na Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Tanzania Health Promotion Support (THPS), Dk. Redempta Mbatia.

Pamoja na huduma za maambukizi kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto, ikijumuisha na matibabu ya VVU, ushauri, kinga na tiba ya magonjwa nyemelezi ikijumuisha TB.

Akifafanua zaidi katika taarifa yake, Mkurugenzi Mkuu THPS, Dk. Redempta, ulisaidia kuwapo maafikiano na Hospitali za Rufani za Mikoa na Wakurugenzi Watendaji wa Halmashauri, rasilimali watu 1,465 katika halmashauri 34, sampuli za usaidizi na kutoa usafiri kwa vituo vya afya 364.

Alisema kuwa mradi wa Afya Hatua (2021-2026), umekuwa ukiunga mkono serikali katika juhudi za kufikia udhibiti wa janga la UKIMWI, kwa kusaidia huduma za kinga, matunzo na matibabu katika jamii katika mikoa ya Kigoma, Pwani, Shinyanga na Tanga, huduma maalum za kinga dhidi ya VVU katika vituo mbalimbali.

Alisema kwamba mradi ulisaidia matibabu ya methadone kwenye kliniki za MAT Pwani na Tanga, pia ulisaidia tohara ya hiari kwa wanaume (VMMC) katika mikoa ya Kigoma na Shinyanga.

Kwa mujibu wa Shirika la Kupambana na Ugonjwa wa Ukimwi la Umoja wa Mataifa (UNAIDS), nchi za Botswana, Eswatini, Rwanda, Tanzania na Zimbabwe zimefikia lengo la '95-95-95'.

Nchi zingine 16 zinakaribia kufikia lengo hilo, zikiwamo nane zaidi katika eneo la Kusini mwa Jangwa la Sahara.

***Kwa maoni kuhusu habari hii: Piga/sms / WhatsApp : +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.co.tz***

HABARI KITAIFA

# Vifurushi vipya NHIF vyapokewa kwa hisia tofauti

**Na Elizabeth Zaya**

VIFURUSHI vipya vya matibabu vilivyotolewa na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) vimepokewa kwa hisia tofauti mitaani, baadhi ya wananchi wakidai ni ghali kwao.

Wamiliki wa vituo binafsi vya kutolea huduma za afya wamesema hawana shida na vifurushi hivyo vipya, wakishauri mfuko utoe elimu kwa wanachama wake kuhusu vifurushi hivyo.

Mwenyekiti wa Umoja wa Vituo Binafsi vya Utoaji Huduma za Afya Tanzania (APHFTA), Dk. Egina Francis, alisema hawana tatizo na vifurushi hivyo vipya, akishauri NHIF kutoa elimu kwa wateja wake ili kupunguza lawama ambazo zinaweza kujitokeza wanapokwenda hospitalini kutibiwa.

Alisema wanachotaka ni kuhakikisha vivurushi hivyo vipya vinawekwa katika mfumo ili mgonjwa anapokwenda hospitalini asihangaike.

Kukiwa na mapokeo hayo ya wadau hao, baadhi ya wananchi waliozungumza kwa nyakati tofauti jana na mwandishi wa habari hi, walidai kuwa kwa namna gharama za matibabu zinavyopanda nchini, kuna hatari kubwa baadhi ya watu wakaamua kutafuta mbadala wa matibabu, ikiwamo kukimbilia kwa sangoma.

"Hii hali ya kila siku vifurushi hivi kupanda kila siku inatisha... kuna wakati walitangaza ile inaitwa Bima ya Afya kwa Wote, tunafikiri kwamba huenda hii ikasaidia kuleta ahueni kidogo, lakini tunaona kama hali inazidi kuwa mbaya. Sasa NHIF wanatutangazia vivurushi vipya, tena gharama yake inazidi kupanda juu.

"Yaani ukiangalia hivi vya sasa ndio kama wanatuchanganya kabisa hadi unatamani kwamba angalau mara mia wangeacha kama vile vilivyokuwapo awali kuliko huku wanakoelekea... wanachotutafutia kwa sasa ni magonjwa ya akili," alidai Anna Joel, mamalishe katika eneo la kibiashara Mwenge, wilayani Kinondoni.

Christopher Thomas, mfanyabiashara wa nguo katika eneo hilo, alisema: "Vifurushi vipya vya NHIF vinamtupa mbali na matibabu mtu mwenye hali ya chini kwa sababu katika mazingira ya kawaida kati ya watanzania milioni 60, ni wachache wenye uwezo wa kupata milioni moja kila mwaka kwa ajili ya tiba.

"Yaani eti mwaka huu nitafute Sh. milioni moja au zaidi hata kama ni Sh. 500,000 halafu mwaka ukiisha nitafute tena nyingine nilipe tena, wakati hata kodi ya nyumba yenyewe ninahangaika nayo kwa tabu kuilipa. Ninaona wanataka tuwe tunajinywea miti shamba tu nyumbani ambayo hatujui hata kama inatibu au inatuua, hebu watuonee huruma.

"Tatizo ni kwamba wanaweka hivi viwango kwa kuwaangalia watu wenye vipato vyao, wakurugenzi, wabunge, watu wenye nafasi zao kubwa maofisini, wanasahau kwamba kuna sisi wa huku tunaodunduliza... wanasahau kwamba kuna mtu anauza karanga kutwa nzima hata kuipata hiyo Sh. 5,000 ni shida halafu eti huyo ndiye apate Sh. 200,000, 500,000 au Sh. milioni 1.5 au na zaidi kwa ajili ya matibabu yake yeye na watoto wake, hii inatisha sana," alilalama.

Judith Kimario, mwanafunzi wa mwaka wa tatu katika moja ya vyuo vikuu vilivyoko Dar es Salaam, alisema ameshangaa kuona katika vifurushi hivyo vipya, hata wazee kuanzia miaka 60 nao wanatakiwa kulipia.

"Nilijua kwamba sheria inasema wazee kuanzia umri huo wanatakiwa watibiwe bure, kwenye vivurushi hivi wanatakiwa walipie, sasa kundi hili wengi wao si ni wastaafu, hizo fedha zote wanazitoa wapi?

"Mbona hii ni hatari, tunaomba vipitiwe upya na ikiwezekana watafute njia nyingine ya kurahisisha huduma za tiba kwa mtanzania, si kwa namna hii ya sasa," alidai Judith.

Mwanaharakati Alfred Mwaijonga alisema kuendelea kupanda kwa gharama za maisha pamoja na kutokuwa na uhakika wa matibabu kwa kukosa bima ya afya ni miongoni mwa vitu vinavyoowaongezea watu maradhi.



"Mnasema watu wanapata vichaa, haya yanasababishwa na mengi, mtu akigeuka huku vifurushi havishikiki, bado hajalipa pango la nyumba, mara sijui bili gani hujalipa, kwa nini usipate kichaa?

"Mimi ningeshauri kwamba serikali iangalie upya namna ya kupanga vifurushi hivi kulingana na vipato vya watu wake ili kila mtanzania awe na uhakika wa matibabu.

"Mimi ninaamini wangetumia hata ule mfumo wa kuchangisha kwa lazima kila mtanzania mwenye simu wamkate hata Sh. 500 kwa mwezi ile fedha ingetosha sana kuwatibu watu wote tena bila tabu," alishauri Mwaijonga.

Vifurushi hivyo vipya ambavyo vimetangazwa na NHIF, viko katika makundi ya aina mbili; Serengeti Afya na Ngorongoro Afya. Kifurushi cha gharama ya chini ni Sh. 240,000 na cha juu ni Sh. 6,388,400.

Kwa mujibu NHIF, watoto wa kuanzia miaka 0-17, mmoja analipa Sh. 240,000 kwa kifurushi cha Ngorongoro na Sh. 660,000 kwa kifurushi cha Serengeti.

***Kwa maoni kuhusu habari hii: Piga/sms / WhatsApp : +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.co.tz***


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA KILIMO**

**MAMLAKA YA UDHIBITI WA NAFAKA NA MAZAO MCHANGANYIKO**

## TAARIFA KWA UMMA

**UFUNGUZI WA MSIMU WA UNUNUZI WA ZAO LA CHOROKO KWA MSIMU 2024/2025 NA UTARATIBU WA USAJILI WA WAKUSANYAJI MAZAO, WAKULIMA WAKUBWA NA VITUO VYA KUKUSANYIA MAZAO**

Msimu wa ununuzi wa zao la choroko kwa mwaka 2024/2025 utafunguliwa rasmi tarehe 29 Januari 2025. Minada itaanza kufanyika kwenye Mikoa ya Mwanza, Simiyu, Shinyanga, Mara na Geita. Taarifa zaidi za minada zitatangazwa kwenye tovuti na kurasa za mitandao ya kijamii za Mamlaka ya Udhibiti wa Nafaka na Mazao Mchanganyiko (COPRA) na Soko la Bidhaa Tanzania (TMX).

Kwa mujibu wa Vifungu vya 4(1), na 4(2) (e), (f), (i), (j) vya Sheria ya Usalama wa Chakula ya Mwaka Sura 249 na Marekebisho yaliyofanywa na Sheria ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko Sura ya 249 , Mamlaka ya Udhibiti wa Nafaka na Mazao Mchanganyiko kwa kushirikiana na Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala (WRRB), Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC) na Soko la Bidhaa Tanzania (TMX) wametoa Maboresho ya Mwongozo wa Biashara kwa Mazao ya Dengu, Choroko, Mbaazi, Soya na Ufuta Toleo la 3 – 2025. Mwongozo huo pamoja na mambo mengine unalenga kulinda ubora wa mazao ya dengu, choroko, mbaazi, soya na ufuta pamoja na kuongeza wigo wa ushiriki na ushindani kupitia minada. Mwongozo huu unapatikana kwenye kiunganishi **https://www.copra.go.tz/publications/guidelines.**

**MATAKWA YA USHIRIKI WA WAKUSANYAJI MAZAO NA WAKULIMA WAKUBWA**

Mwongozo huo umeainisha ukusanyaji wa mazao kwa Njia kuu mbili ambapo mazao yatakusanywa kupitia ushirika au kupitia wakusanyaji /wakulima wakubwa waliosajiliwa na COPRA. Ili washiriki kwenye biashara ya mazao hayo, wakusanyaji mazao/wakulima wakubwa, mwongozo umeweka taratibu zifuatazo.

1. Kuwa na leseni ya biashara;
2. Kujisajili na COPRA kupitia kiunganishi cha **asds@kilimo.go.tz** au maafisa wa COPRA walio katika ofisi za mikoa/kanda husika
3. Kutambulisha vituo vya kukusanyia mazao watakavyovitumia kwa COPRA;
4. Kununua mazao kutoka kwa wakulima kwa bei isiyopungua **bei elekezi** itakayokua inatangazwa na COPRA kila wiki; na
5. Kufuata taratibu zote zilizowekwa kwenye Mwongozo wa Biashara kwa Mazao ya Dengu, Choroko, Mbaazi, Soya na Ufuta Toleo la 3 – 2025 pamoja na kiambatisho chake Na. 1 vinavyopatikana kupitia kiunganishi cha **https://www.copra.go.tz/publications/guidelines.**

**URASIMISHAJI WA GHALA**

Wakusanyaji wa mazao na wakulima wakubwa **wataruhusiwa kurasimisha ghala zao** ili zitumike kama ghala kuu za minada **iwapo zitakidhi vigezo** vilivyowekwa na Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala. Vigezo hivyo vinapatikana kupitia kiunganishi **https://www.wrrb.go.tz/publications/forms.**

Wakulima na wadau wengine watakaoendelea kutumia mfumo wa ushirika wataendelea kukusanya mizigo yao kupitia Vyama vya msingi (AMOCs) na baadae kwenda ghala kuu ambapo minada itafanyika.

**MATAKWA KWA WANUNUZI**

Kwa upande wa wanunuzi watakaoshiriki kwenye minada, **watatakiwa kujisajiliwa na COPRA** na kuweka kinga ya dhamana kama ilivyoainishwa katika Maboresho ya Mwongozo wa Biashara kwa Mazao ya Dengu, Choroko, Mbaazi, Soya na Ufuta Toleo la 3 – 2025, kupitia Soko la Bidhaa Tanzania TMX kwa utaratibu utakaowekwa na Soko hilo. Wanunuzi wadogo wanaweza kushiriki minada kwa kupunguziwa dhamana ili kuchochea ushiriki wa wazawa kwenye biashara hiyo ya mazao.

**KUKIDHI MATAKWA YA KUSAFIRISHA MAZAO NJE YA NCHI**

Kupitia mwongozo huo itambulike kuwa vibali vya kusafirishia mazao nje ya nchi (Export Permit) vitakatolewa kwa mizigo ambayo mauzo yake yamepita kwenye mfumo wa stakabadhi za ghala na minada ya kidijitali pekee.

Kwa muktadha huo, umma unatangaziwa kuwa ni **marufuku kununua zao la choroko pasipo kufuata taratibu zilizowekwa katika Mwongozo wa Biashara kwa Mazao ya Dengu, Choroko, Mbaazi, Soya na Ufuta Toleo la 3 – 2025.** Aidha, msafirishaji wa zao la Choroko atatakiwa kuwa na **Hati ya utoaji wa mazao ghalani** inayopatikana mara baada ya mnada kufanyika na malipo kwa wakulima kufanyika.

Kwa maelezo ya ziada tafadhali wasiliana nasi kupitia barua pepe: **info@copra.go.tz.**

Imetolewa na:

Irene M. Mlola
**MKURUGENZI MKUU**

*Jengo la Kahawa Plaza, Mtaa wa Njedengwa, S.L.P 2780, Dodoma -Tanzania.*
*Simu: +255 26 2310225, Barua pepe: info@copra.go.tz.*

183594

# Neema yaja shule jirani na makaburi

- DED atoa fungu la dharura kujenga miundombinu mipya
- Aipatia vifaa kumalizia mradi ulioanzishwa na wanakijiji

**Na Sanula Athanas**

SIKU chache baada ya Nipashe kuchapisha ripoti kuhusu madhila yanayowakumba wanafunzi na walimu wa Shule ya Msingi Lipumba kutokana na kujengwa jirani na makaburi, uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga, mkoani Ruvuma umechukua hatua za dharura kukabili hali hiyo.

Kwa siku tatu mfululizo kuanzia Desemba 16 hadi 18 mwaka jana, gazeti hili lilichapisha ripoti maalumu ikiangazia madhara ya shule hiyo kujengwa jirani na makaburi ya kijiji.

Mwenyekiti Msaidizi wa Kamati ya Shule hiyo, Remista Ndunguru, katika mazungumzo na mwandishi wa habari hii juzi, alisema kuwa Januari 17 mwaka huu, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga, Joseph Kashushura alizuru shuleni Lipumba kujionea kilichoripotiwa na Nipashe.

"Mkurugenzi alikuja shuleni akiwa na wasaidizi wake. Walipofika, walikagua mazingira ya shule kisha wakawa na mazungumzo na uongozi wa shule, kijiji, parokia na baadhi ya wazee wa kijiji hiki ambao aliagiza wafike kumweleza historia ya makaburi yaliyo jirani na shule," alisema.

Mwenyekiti Msaidizi Remista alisema kuwa baada ya mazungumzo hayo na wazee wa kijiji, Mkurugenzi Kashushura alitoa maagizo matano kwa uongozi wa kijiji cha Lipumba na Kamati ya Shule hiyo ambayo alielekeza utekelezaji wake uanze siku hiyo hiyo (Januari 17, 2025).

Mosi; Uzikaji katika eneo la makaburi karibu na mpaka wa shule usifanyike tena. Miili izikwe katika makaburi hayo, lakini mbali na mpaka wa shule hiyo.

Pili; wanakijiji wasikatishe shuleni wakati wa kwenda makaburini na wakati wa kutoka makaburini.

Tatu; madarasa mawili ya Shule ya Msingi Lipumba yenye uchakavu mkubwa yasitumike tena kwa sababu yanaweka hatarini usalama wa wanafunzi na walimu.

Nne, ujenzi wa madarasa mawili na ofisi ya walimu uanze mara moja shuleni Lipumba na miundombinu hiyo ijengwe mbali na mpaka wa makaburi na shule.

Tano; mkutano wa dharura wa kijiji uitishwe ili kuwaomba wanakijiji washiriki katika ujenzi huo (madarasa na ofisi ya walimu). Halmashauri inachangia Sh. milioni 50.

"Muda mfupi baada ya mkurugenzi na timu yake kuondoka shuleni, sisi Kamati ya Shule tuliona kumewekwa Sh. milioni 50 katika akaunti ya shule," alisema Remista huku akipongeza Nipashe kwa kuripoti kilichokuwa kinajiri shuleni Lipumba.

Remista aliendelea kueleza kuwa siku mbili baadaye (Januari 19, 2025) kuliitishwa mkutano wa kijiji ambao wanakijiji walipewa taarifa kuhusu ziara ya uongozi wa halmashauri na hoja ya ushiriki wao katika ujenzi wa miundombinu mipya ya Shule ya Msingi Lipumba.

Alisema iliridhiwa katika mkutano huo kila mwanakijiji mwenye umri wa kuanzia miaka 18 hadi 50, ashiriki ujenzi huo kwa kununua matofali matano ya saruji, matofali 3,500 yanatarajiwa kununuliwa na wakazi 700 wa kijiji cha Lipumba wenye umri wa kuanzia miaka 18 hadi 50.

Kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022, kijiji hicho kina wakazi 2,198 (wanaume 1,071 na wanawake 1,127), lakini kwa tathmini ya mkutano wa dharura wa kijiji ulioitishwa Januari 19 mwaka huu, kama ilivyotolewa ufafanuzi na Remista, ni wakazi 700 pekee wanaopaswa kununua matofali hayo, vigezo vikuu vilivyozingatiwa ni umri na uwezo wa kufanya kazi.

"Nguvu ya wananchi inahitajika kufanikisha ujenzi huu maana Sh. milioni 50 zilizotolewa na halmashauri, kwa hesabu iliyofanyika katika mkutano wa kijiji, ilionekana zinatosha kununua vifaa vya viwandani tu. Mchanga, kokoto na mbao lazima nguvu za mwananchi zitumike.

"Tumekubaliana matofali yanunuliwe kwa mzalishaji mmoja ili yasipishane mkubwa na ubora. Utaratibu unaotumika sasa, wananchi wanaungana, wakishafika 20 wanapeleka fedha kwa mzalishaji, matofali yao yanaletwa shuleni. Kwa huyo mzalishaji tofali moja anauza Sh. 2,300 pamoja na usafiri kutoka mjini Mbinga hadi hapa shuleni. Mwisho wa kuleta matofali shuleni ni Februari 10, mwaka huu," Remista alisema.

Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Lipumba, Mathias Mpangala, alithibitisha taarifa iliyotolewa kwa Nipashe na Mwenyekiti Msaidizi Remista na kuongeza kuwa mbali na kuwekwa Sh. milioni 50 katika akaunti ya shule, Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga pia imewapatia vifaa vya kumalizia mradi wa darasa lenye vyumba viwili na ofisi ya walimu linalojengwa na wanakijiji shuleni Lipumba.

"Juzi (Jumamosi) mkurugenzi alileta mifuko 70 ya saruji, mabati matano ya kumalizia kofia ya darasa linalojengwa kwa nguvu za wananchi. Pia ameleta mchanga laini tripu mbili za lori na tripu mbili zingine za mchanga mgumu kwa ajili ya kumalizia kupiga lipu lile darasa na ofisi.

"Wananchi wameupokea vizuri mradi huu wa ujenzi wa madarasa. Zilipotolewa zile Sh. milioni 50, hesabu ilionesha kujenga madarasa mawili na ofisi ya walimu, zile fedha zisingetosha. Zingeishia kwenye baadhi ya vifaa tu, ndiyo maana wameamua kuchangia ujenzi wa madarasa hayo kwa kununua matofali yote ya ujenzi," alisema.

Katika kusimamia ujenzi huo wa madarasa na ofisi ya walimu, Mpangala alisema wana kamati mbili: Kamati ya Shule inasimamia matumizi ya Sh. milioni 50 zilizotolewa na halmashauri na Kamati ya Kijiji iliyoundwa ikiwa na wawakilishi wawili kwa kila kitongoji; wanasimamia ununuzi wa matofali. Kila mwanakijiji atakayenunua matofali, atathibitishwa na kamati hiyo ya kijiji.

"Tunatarajia kuanza ujenzi wa madarasa mapya muda wowote. Kinachosubiriwa sasa ni taarifa ya wahandisi kutoka halmashauri ambao hivi karibuni walikuja shuleni kupima eneo la shule ili kuchagua eneo sahihi la kujenga madarasa hayo. Lengo letu ni kuondoka kule karibu na makaburi na mkurugenzi amesisitiza tujenge mbali zaidi na makaburi," Mpangala alisema katika mazungumzo na mwandishi wa habari hii jana.

**UFAULU DUNI**

Kama ilivyokuwa kwa matokeo ya Mtihani wa Darasa la Saba mwaka jana, Shule ya Msingi Lipumba haijafanya vizuri katika Mtihani wa Taifa wa Upimaji Darasa la Nne Mwaka 2024.

Kwa mujibu wa matokeo hayo yaliyotangazwa Januari 4, 2025 na Katibu Mtendaji wa Baraza la Mitihani la Taifa (NECTA), Dk. Said Mohamed, Shule ya Msingi Lipumba ilikuwa na watahiniwa 52. Kati yao, hakuna aliyefaulu kwa daraja "A" wala "B", 15 wamepata daraja "C", 33 daraja "D" na wamefeli, kwa maana wamepata daraja "E", hivyo wanapaswa kukariri darasa.



Mchanga uliopelekwa shuleni Lipumba jana

| JINSI | A | B | C | D | E |
|---|---|---|---|---|---|
| WAS | 0 | 0 | 12 | 15 | 1 |
| WAV | 0 | 0 | 3 | 18 | 3 |
| JUMLA | 0 | 0 | 15 | 33 | 4 |

Mchanganuo wa matokeo ya Mtihani wa Taifa wa Upimaji Darasa la Nne Mwaka 2024 katika Shule ya Msingi Lipumba. **CHANZO: NECTA, Januari 4, 2025**



Sehemu ya madarasa ya Shule ya Msingi Lipumba jirani na makaburi ya kijiji

# Injini za Airbus zaitia hasara ya bilioni 127/- ATCL kila mwaka

**Na Augusta Njoji,**
DODOMA

LICHA ya mafanikio yanayopatikana kwenye Shirika la Ndege Tanzania (ATCL), Kamati ya Bunge ya Miundombinu imesema matatizo ya kiusanifu ya injini za Airbus A220-300 ambazo zimekuwa zinapata hitilafu mara kwa mara, yanasababisha kukosa mapato wastani wa Sh. bilioni 127.3 kwa mwaka.

Akiwasilisha bungeni jana taarifa ya mwaka ya kamati hiyo kwa kipindi cha Februari 2024 hadi Januari 2025, Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Moshi Kakoso, alishauri serikali iharakishe upatikanaji injini mbadala za ndege aina ya A220-300 na pia itafute namna bora ya kuhakikisha ndege hizo zinaleta faida kwa nchi.

Mwenyekiti huyo alitaja changamoto nyingine ni upatikanaji vipuri kutokana na kushuka kwa uzalishaji vipuri hivyo duniani kutokana na athari za UVIKO-19.

Alisema ATCL pia inakabiliwa na uhaba wa marubani, hususan marubani viongozi, na wahandisi wenye leseni ya kuruhusu ndege kuruka baada ya matengenezo kukamilika.

Vilevile, kiongozi huyo wa kamati alisema kuna madeni yanayotokana na mkataba wa ukodishaji ndege kati ya ATCL na TGFA. Deni ya nyuma la TGFA ni Sh. bilioni 429 hadi Juni, 2024 na deni la taasisi za serikali ni Sh. bilioni 64 huku madeni ya wazabuni yakiwa Sh. bilioni 18.

"Serikali ifute deni la TGFA la Sh. bilioni 429, isimamie taasisi nyingine za serikali kulipa Sh. bilioni 64 kwa ATCL na kulipa madeni ya wazabuni Sh. bilioni 18 ili kuondoa changamoto ya madeni ya nyuma yanayolikabili shirika," alisema.

Mwenyekiti huyo alishauri serikali iendelee na mchakato wa kuhamisha ndege kutoka TGFA kwenda ATCL na isimamie kuboreshwa sheria ya uanzishwaji ATCL ili itambulike kama kampuni badala ya shirika la umma.

**UTAPELI MTANDAONI**

Vilevile, alisema suala la utapeli na uhalifu mwingine wa kimtandao limeendelea kuwa tatizo nchini, jambo linalopaswa kupatiwa ufumbuzi wa kina.

"Serikali iimarishe udhibiti wa uhuru wa mitandao kwa kuzingatia umuhimu wa demokrasia yenye mipaka; ihakikishe TCRA kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi, inaweka mikakati madhubuti inayozihusisha kampuni za simu kukabiliana na uhalifu wa kimtandao," alisema.

Aliongeza kuwa katika kudhibiti uhalifu wa mitandao ya mawasiliano, serikali inapaswa kuhakikisha kampuni za simu zinawajibika ipasavyo katika kutoa nafuu za kisheria kwa waathirika wa uhalifu wa kimtandao.

**MADENI POSTA**

Kakoso pia aliitaka serikali ibebe deni linalodaiwa na Shirika la Posta Tanzania la Sh. bilioni 54 ili kusafisha mizania ya shirika na kuliwezesha kujiendesha... kopesheka.

Alisema serikali inapaswa pia kuongeze kasi ya kutekeleza ujenzi wa minara ya mawasiliano, hasa maeneo yaliyoainishwa kuwa na mahitaji maalum, akitolea mfano barabara kuu, mbuga za wanyama, mipakani na mapori tengefu ili kukuza shughuli za utalii na kuboresha usalama.

# Miaka 48 ya CCM kutumika mkakati wa wagombea urais

**Na Augusta Njoji,**
DODOMA

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) kimesema katika maadhimisho ya miaka yake 48 yatakayofanyika kesho jijini Dodoma, wagombea wa nafasi ya urais watatambulishwa kwa wanachama wake, huku kikiwa na turufu ya ushindi mnono Uchaguzi wa Serikali za Mitaa na utekelezaji wa Ilani yake.

Wagombea hao waliopitishwa kwenye Mkutano Mkuu Maalum hivi karibuni ni Samia Suluhu Hassan kwa nafasi ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mgombea Mwenza, Balozi Dk. Emmanuel Nchimbi na kwa upande wa Zanzibar atatambulishwa Dk. Hussein Ali Mwinyi.

Chama hicho kimesema kinaamini falsafa ya 4R ambazo ni Resilience (ustahimilivu), Rebuild (kujenga upya), Reform (mabadiliko), Reconciliation (maridhiano) itasaidia vyama vya siasa kufanya siasa hata kama wanatofautiana kiitikadi, lakini nchi itaendelea kubaki salama.

Akizungumza jana na waandishi wa habari jijini hapa, Katibu wa Halmashauri Kuu ya CCM Taifa, Itikadi, Uenezi na Mafunzo, Amos Makalla, alisema pamoja na shughuli zilizopangwa kufanyika watatumbulisha wagombea wao watakaopeperusha bendera ya CCM katika uchaguzi mkuu na kueleza mafanikio yaliyopatikana.

"Tunajua muda haujafika wa kuwatambulisha kwa wananchi, hapa tunawatambulisha kwa wanachama wa CCM kutokana na sherehe hizi za kuzaliwa CCM wanachama watatambulishwa wagombea wao," alisema.

Makalla alisema chama hicho kinaadhimisha miaka 48 kikiwa ni imara chenye wanachama milioni 12 na chenye serikali na kikiwa kimeshinda uchaguzi wa Serikali za Mitaa uliofanyika mwaka 2024 kwa asilimia 98.

"Tunajivunia amani na utulivu chini ya serikali mbili zilizopo, nchi yetu ina amani na utulivu pamoja na uwapo wa vyama nchi yetu tunaendelea kuongozwa na falsafa ya 4R katika kufanya siasa. Ndio maana chama cha Mapinduzi kinaamini kuwa 4R zitasaidia sana kwa vyama vya siasa kuendelea kufanya siasa tukitofautiana kiitikadi, lakini nchi yetu ikibaki kuwa salama," alisema.

Alisema sherehe hizo zitaongozwa na Rais Samia.


NSSF
Tunajenga Maisha Yako ya Sasa na Baadaye

TAARIFA KWA UMMA

ZOEZI LA UHAKIKI WA WASTAAFU NA WATEGEMEZI

Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) unawatangazia wastaafu na wategemezi wote wanaolipwa pensheni ya kila mwezi kuwa, kutakuwa na zoezi la uhakiki litakaloanza tarehe **3 Februari, 2025** hadi **30 Aprili, 2025.** Zoezi hili litafanyika Jumatatu hadi Ijumaa kuanzia saa 2:30 asubuhi hadi saa 10:30 jioni kwenye ofisi zote za NSSF. Kwa wastaafu waliopo Unguja na Pemba, uhakiki wao utafanyikia ofisi ya ZSSF. Aidha kwa wastaafu waliopo Dar es Salaam, uhakiki wao utafanyika katika ofisi za mikoa ambazo ni **ILALA, TEMEKE, KINONDONI, UBUNGO, MBEZI BEACH na KIGAMBONI**

**Mstaafu ambaye atatembelea ofisi za NSSF anatakiwa kufika na nyaraka zifuatazo:**

i) Kitambulisho cha NSSF au kuponi ya pensheni,
ii) Kitambulisho cha Taifa au namba ya NIDA,
iii) Picha moja ndogo ya sasa (passport size) kwa wale ambao hawakufanya uhakiki kwa mwaka 2024,
iv) Kwa wategemezi (Watoto) tafadhali fika na cheti cha kuzaliwa na kitambulisho cha shule
v) Kwa wastaafu wagonjwa au wazee wasiojiweza taarifa itolewe kupitia barua pepe **customercare@nssf.go.tz** au kwa kupiga simu ya bure **0800116773** au kuwasilisha taarifa husika kwenye ofisi ya NSSF iliyo karibu

Kwa wastaafu ambao wameshawasilisha namba za NIDA katika Mfuko wanaweza kujihakiki wenyewe kupitia simu zao za kiganjani

**ANGALIZO:**

Malipo ya pensheni ya mwezi **Julai 2025** yatafanyika kwa wastaafu na wategemezi ambao wamehakiki tu

**ATAKAYESIKIA TANGAZO HILI AMTAARIFU NA MWENZAKE**

Imetolewa na:
**Kitengo cha Uhusiano na Elimu kwa Umma**

Pensheni ya Uzee | Pensheni ya Ulemavu | Pensheni ya Urithi | Mafao ya Uzazi | Msaada wa Mazishi | SHIB | Mafao ya Kukosa Ajira

@NssfTanzania | www.nssf.go.tz

183591

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kamati kuchunguza wageni wanaofanya 'umachinga' Kariakoo taarifa ije kwa wakati

**KUMEKUWA** na malalamiko ya wageni wanaoingia nchini kwa lengo la kufanya uwekezaji, lakini huishia kufanya kazi za uchuuzi zinazofanywa na wazawa ikiwamo kuuza biashara ndogo ndogo maarufu 'machinga'.

Wageni hao wamekutwa maeneo mbalimbali ya majiji nchini, likiwamo la Kariakoo wakitangaza biashara zao ambao hutandazwa chini kama wanavyofanya wafanyabiashara wazawa, hali inayozua maswali iweje watu wanaojiita wawekezaji kufanya biashara ndogo ndogo.

Kutokana na malalamiko hayo, hivi karibuni Waziri wa Viwanda na Biashara, aliunda kamati maalumu ya watu 15 kuchunguza wimbi la wageni kufanya biashara za uchuuzi 'Umachinga' katika Soko la Kariakoo, Dar es Salaam na maeneo mengine.

Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, alisikia kilio cha Watanzania hususan wafanyabiashara wa Kariakoo, kuhusu kero hiyo.

Kamati hiyo itafanya kazi hiyo ndani ya mwezi mmoja na kuwasilisha taarifa yake.

Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, alipokea kilio cha wananchi wa Kariakoo, Dar es Salaam na Watanzania hususan wafanyabiashara, suala la hivi sasa kuwapo kwa mwingiliano wa wageni wengi ambao huwa wanakuja na ajenda ya uwekezaji, kwa bahati mbaya uwekezaji wao hauakisi suala zima la uwekezaji.

Baadhi ya shughuli hizo hususan ni kufanya biashara za rejareja za kimachinga, mwisho wa siku huathiri mwenendo wa biashara kwa Watanzania.

Hali hiyo inaathiri biashara zao huku ikizingatiwa Tanzania inaendeshwa kwa mujibu wa sheria, taratibu na kanuni ambapo mgeni yeyote au mtu anapaswa kufanya biashara kulingana na maelekezo ya serikali.

Kuna wimbi la wageni ambao wanafanya biashara tofauti na utaratibu wa kisheria, hivyo huleta kero kwa wafanyabiashara wazawa na kuathiri mitaji yao na kuwa na vijana waliofilisika kutokana na wengine kuanzisha magodauni na kuleta biashara na kuuza rejareja.

Miongoni mwa hadidu za rejea ni utafiti wa kina Soko la Kariakoo likiwa kama la mfano, kubaini ukubwa wa tatizo la wageni kufanya biashara nchini ambalo linaathiri ajira kwa Watanzania.

Pia, watakagua vibali vya wageni na uhalali wake, kuchunguza wageni kupewa vibali na leseni za biashara zinazofanywa na Watanzania.

Kamati hiyo itaangalia masuala ya dharura ni nini kifanyike kwa haraka kutatua tatizo hilo kwa kuainisha njia za haraka na muda mfupi, chanzo cha tatizo na namna ya kuepuka.

Wakati kamati hiyo ikifanyakazi yake wafanyabiashara wametakiwa kuwa watulivu ili matokeo ya kazi hiyo yasaidie sio tu sekta ya biashara bali na nyingine kuweka misingi ya utekelezaji.


Mwenyekiti wa Soko la Kariakoo, alisema kutokana na maelekezo ya Rais Dk. Samia changamoto ya uwapo wa wageni kufanya biashara za uchuuzi itapatiwa ufumbuzi.

Hatua hii ya kufanya uchunguzi wa malalamiko ya wafanyabiashara haina budi kuungwa mkono kwa kuwa serikali imechukua uamuzi ndani ya muda mfupi baada ya kutolewa kwa maelekezo na kuundwa kamati hiyo ambayo imepewa siku 30 kuwasilisha mapendekezo ya nini kifanyike.

Kikubwa kinachosubiriwa na matokeo ya uchunguzi huo ili ukubwa wa tatizo hilo uweze kubainika na hatua za haraka zichukuliwe kunusuru wafanyabiashara wa ndani wasiathirike katika shughuli zao na kuweza kulipa kodi kama sheria inavyotaka.

Kila la heri kamati iliyoundwa ni matumaini ya wengi kuwa kazi hiyo itafanyika kwa wakati.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Sabato Kasika

## Muungwana Lazima Nilonge

# Hongera Chuo cha Ustawi wa Jamii kwa programu hii

**CHUO** cha Ustawi wa Jamii, kinaendesha programu mbalimbali ikiwamo ya kutatua matatizo yanayoikabili jamii, hasa kwa upande wa malezi na makuzi ya watoto na vijana.

Hatua hiyo inatokana na kile kinachoelezwa na uongozi wa chuo kuwa ni baada ya kuona kuna hitaji hilo, kufuatia kuwapo kwa matukio ya ukatili wa kila aina kuanzia mauaji, ulawiti, ubakaji na vipigo.

Ili kupunguza au kumaliza matatizo hayo ndani ya jamii, chuo kinaona njia mojawapo ya kuyakabili ni programu ya malezi na makuzi ya watoto kwa lengo la kuwa na kizazi bora cha baadaye.

Kinachoelezwa na uongozi wa chuo ni sahihi, kwani sio siri kwamba maadili ndani ya jamii yameporomoka, matukio ya ukatili yamekuwa kama sehemu ya maisha ya kila siku.

Hivyo, programu hiyo imekuja wakati sahihi ili kusaidia kuelimisha vijana na jamii kwa ujumla kujua umuhimu wa maadili mema ili kuondokana na vitendo hivyo vinavyohatarisha maisha ya watu.

Mkuu wa chuo hicho, Dk. Joyce Nyoni katika maelezo yake, anasema utaratibu unaotumiwa na chuo ni ushirikishwaji wa jamii kwa kuchangamana nayo ili kujifunza na kufanya kazi nayo.

Anafafanua kuwa utaratibu huo una mchango mkubwa wa wahitimu wa chuo kupata nafasi ya kuunganisha nadharia ya darasani na uhalisia kwenye jamii ili kupata jibu la kumaliza matatizo hayo.

Kama anavyoeleza mkuu wa chuo, kuwa kutokana na mahitaji hayo, wameamua kujikita katika kuandaa wataalamu ambao ni sehemu muhimu ya makuzi na malezi ya watoto na vijana, hiyo ni hatua nzuri.

Sio siri kwamba ndani ya jamii kuna mmomonyo mkubwa wa maadili, kama nilivyoeleza, hivyo, bila kuwapo jitihada mbalimbali za kunusuru kizazi kijacho, taifa la baadaye linaweza kuwa la watu wa ajabu.

Ninadhani ni vyema jamii ikawa tayari kuungana na wasomi wa chuo hicho watakaowafikia huko mitaani ili kusaidia kuelezea changamoto zinazochangia kuwapo kwa vitendo vya ukatili katika jamii.

Kwa njia hiyo, inaweza kuwa rahisi au kusaidiwa jamii kurudi kwenye mstari na kuzingatia malezi na makuzi ambayo hayaendi kinyume na mila na desturi za Kitanzania ambazo zimeanza kuharibiwa.

Kuvunjika kwa maadili katika familia na ndani ya jamii kwa ujumla, ni mojawapo ya sababu zinazotajwa kuchangia kwa kiwango kikubwa kutokea kwa wimbi la vitendo vya ukatili wa kijinsia na unyanyasaji.

Imekuwa ni jambo la kawaida kwa baadhi ya watu wazima na vijana kusambaza picha za ngono kupitia mitandao ya kijamii ambazo wakati mwingine zinatazamwa na watoto wadogo.

Hivyo, kwa kuwa chuo hicho kimeamua kutojikita katika taaluma ya darasani na pia kwenda kufanya kazi ndani ya jamii, ninadhani ni vyema programu hiyo iungwe mkono ili ilete matokeo chanya.

Ni vyema wazazi, walezi na jamii kwa ujumla, wawe tayari kushirikiana na wataalamu kutoka chuo hicho, ili kile ambacho kimekusudiwa kufanywa kiweze kuwafikia walengwa wote ili kuokoa kizazi kijacho.

Inawezekana wazazi, walezi wameshindwa kuchukua hatua za kusimamia malezi mema na kusabisha watoto wao wajiingize katika vitendo vya mmomonyoko wa maadili.

Lakini kupitia programu ya Chuo cha Ustawi wa Jamii, inawezekana kuwa na mabadiliko makubwa ya kurudisha jamii kwenye mstari iwapo jamii itaipa uzito wa kutosha kwa kutoa ushirikiano.

## Kampeni ya msaada wa kisheria yamaliza mgogoro wa ndoa uliodumu miaka minne

**Na Elizabeth Zaya**

KAMPENI ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia ambayo imefanyika kwa siku tisa katika mikoa sita imetatua changamoto mbalimbali katika jamii, ikiwamo kumaliza mgogoro wa ndoa uliodumu kwa miaka minne wilayani Kakonko, mkoani Kigoma.

Wanandoa hao kutoka kijiji cha Rumashi wilayani humo waliingia katika mgogoro huo huku chanzo kikitajwa kuwa ni mmoja wao kushindwa kutoa huduma ya msingi ya ndoa kwa mwenzake.

Maofisa wa kampeni hiyo walifanikiwa kutatua mgogoro huo baada ya mmoja wa wanandoa hao, Dativa Kachira kujitokeza mbele yao akiomba msaada huo wa kisheria.

Dativa alidai kuwa kutokana na mgogoro huo uliodumu wa muda mrefu, amekuwa anapitia madhila ikiwamo mume wake kushindwa kumpatia mahitaji ya nyumbani na ya watoto shuleni.

Alidai kuwa kutokana na hali hiyo, yeye na wanawe walikuwa wanapitia wakati mgumu kwa miaka yote hiyo na hata kukwamisha na kurudisha nyuma maendeleo ya watoto wao kimasomo.

"Mume wangu ana uwezo mzuri tu wa kuhudumia familia na ikaishi vizuri, lakini kwa kipindi chote hicho hafanyi chochote kwa makusudi tu na ndiyo maana niliposikia kuna msaada wa kisheria, ikanilazimu nije nimshtaki kwa sababu hali imezidi kuwa mbaya kwenye familia yangu," alidai Dativa.

Alidai amekuwa anakwenda mara kwa mara kumshtaki kwenye mamlaka za serikali katika eneo hilo wanaloishi, lakini hajapata ufumbuzi.

Akizungumza mbele ya maofisa kwenye kampeni hiyo, mume wa Dativa, Stides Stephano, alimtupia lawama mkewe huyo, akidai ndiye alianzisha mgogoro huo kwa kuwafukuza nyumbani watoto aliokuwa amezaa na mwanamke mwingine.

Stephano alidai kuwa alikuwa anamnyima chakula na huduma nyingine nyumbani ambazo ni haki yake kupewa. Alidai mkewe huyo, aliuza mazao yote waliyolima na hakumpatia fedha yoyote.

Mratibu wa Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia Wilaya ya Kakonko, Jackline Kulwa, alisema kuwa baada ya mazungumzo na usuluhishi, wanandoa hao walisameheana na kukubaliana kuishi kwa amani na kutunza familia yao.



Mkurugenzi wa Tasisisi ya Sibusiso Foundation, Martha Lukas, akitoa shukrani kwa Benki ya Stanbic Tanzania, baada ya kupokea msaada wa meza 20 kwa ajili ya kituo hicho, kinacholea watoto wenye ulemavu wa mtindio wa ubongo jijini Arusha jana. Msaada huo, ni sehemu ya mpango wa benki hiyo kurudisha kwa jamii utawawezesha watoto hao kuwa na mazingira mazuri ya kujisomea. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Serikali yaongeza vituo maalum vya selimundu

## •Waliopandikizwa uloto nchini wafikia 27

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imeliarifu Bunge kuwa imeongeza vituo maalum vya selimundu (sikoseli) kutoka vituo vinane mwaka 2021 hadi vituo 45 Januari 2025.

Naibu Waziri wa Afya, Dk. Godwin Mollel alibainisha hayo jana bungeni jijini Dodoma alipojibu swali la Mbunge wa Mwanakwerekwe (CCM), Hassan Haji Kassim aliyetaka kujua lini serikali itaongeza kasi ya upatikanaji huduma kwa watu wenye magonjwa ya

damu kama vile himofilia na selimundu.

Himofilia ni ugonjwa wa kutokwa damu bila kukoma unapopata jeraha wakati selimundu ni ugonjwa wa kuzaliwa nao kutokana na kuurithi kutoka kwa wazazi kupitia vinasaba ambapo baadhi ya seli nyekundu za damu huwa na umbo lisilo la kawaida. Badala ya kuwa na umbo linalofanana na diski, zinakuwa na umbo kama la nusu mwezi ambalo husababisha seli nyekundu za damu kuvunjika kwa urahisi na zisitoshee vizuri katika mishipa midogo ya damu ili kusafirisha oksijeni.

Akijibu swali la mbunge huyo, Dk. Mollel alisema vituo hivyo vinajumuisha Hospitali ya Taifa ya Taifa Muhimbili (MNH), hospitali sita za kanda, hospitali 28 za mikoa na hospitali 10 za wilaya.

Naibu Waziri Dk. Mollel alisema kuwa hadi kufikia Januari 2025, jumla ya vituo 13 vimewezeshwa kutoa huduma za himofilia kutoka vituo saba mwaka 2021, sawa na ongezeko la asilimia 49.5.

Pamoja na hayo, Dk. Mollel alisema serikali imewajengea uwezo madaktari bingwa wa watoto (324), madaktari bingwa wa magonjwa ya ndani na madaktari bobezi wa magonjwa ya damu (60) ambao ni sehemu muhimu katika utoaji huduma za sikoseli na himofilia.

"Serikali imeanzisha huduma za upandikizaji uloto kwa wagonjwa wa sikoseli katika Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Benjamin Mkapa (BMH). Hadi kufikia Januari 2025, jumla ya wagonjwa 27 walipatiwa huduma hiyo," alisema.

Alisema wagonjwa wote hao wamepatiwa huduma kwa ufadhili kupitia Mfuko wa Rais Samia Suluhu Hassan. Gharama za upandikizaji uloto katika hospitali hiyo ni kati ya Sh. milioni 50 na milioni 55 kwa mgonjwa.

Katika swali la nyongeza, Mbunge Kassim alihoji mkakati wa serikali kufanya uchunguzi kwa wajawazito kama ilivyo kwa magonjwa mengine ili kujua chanzo cha ugonjwa husika kwa kuwa magonjwa hayo ni ya kurithi.

"Kwa kuwa kuna ongezeko la magonjwa hayo, ni upi mkakati wa serikali kuongeza huduma ya dawa ili kuwahudumia wagonjwa hao?" Mbunge Kassim alihoji.


Dk. Mollel, akijibu maswali hayo, alisema serikali imeendelea kuwajengea uwezo madaktari bingwa wa watoto ili kutoa huduma bora kwa wajawazito na kuwafuatilia watoto wanapozaliwa na ukuaji wao ili kubaini ugonjwa huo.

Alisema dhamira ya serikali ni kuhakikisha huduma hizo zinafika kwenye hospitali za wilaya zote na baadaye kwenye vituo vya afya.

Takwimu za Wizara ya Afya zinaonesha kila mwaka kuna wastani wa watoto 14,000 wanaozaliwa wakiwa na selimundu nchini, nusu yao hufariki dunia ndani ya miaka mitano ya kuzaliwa kwao.

## KABWELA

FADHILI MOHAMED



# Daktari aliyesimamishwa kazi miaka saba arejeshwa kazini

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

OFISI ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora imeamuru kurejeshwa kazini Dk. John Amita wa Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni, mkoani Singida aliyesimamishwa kazi miaka saba iliyopita kwa tuhuma za kuchelewa kumfanyia upasuaji mjamzito na kusababisha kifo chake.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Simbachawene, akizungumza juzi mjini Singida, alisema amechukua uamuzi huo baada ya kujiridhisha kusimamishwa kazi kwa daktari huyo hakukuzingatia taratibu.

"Tupo kwenye mchakato wa kumwombea Dk. Amita arejeshwe kwenye utumishi wa umma, lakini sasa amekaa benchi miaka saba, hivyo tutamwombea kwa Katibu Mkuu Kiongozi aingie kwenye ajira kwa mkataba," alisema.

Simbachawene, akizungumzia sakata la mtumishi huyo, alisema alituhumiwa kuchelewa kumfanyia operesheni mama mjamzito na kusababisha kifo chake kisha mwajiri wake ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni kuamua kumsimamisha kazi.

Alisema mkurugenzi huyo alichukua uamuzi huo bila kuzingatia kwamba suala hilo ni la kitaaluma. Alipaswa kuvishirikisha vyombo vya kitaaluma au Bodi ya Madaktari, lakini akaamua kumsimamisha kazi bila hata Mkuu wa Wilaya na Katibu Tawala Wilaya kufahamu kama linawahusu.

Simbachawene alisema kuwa baada ya uamuzi huo wa mkurugenzi, Dk.Amita alikata rufani Tume ya Utumishi wa Umma; nayo ilipitia nyaraka ilizopelekewa ikarudisha suala hilo kwa Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni kushauri iundwe timu kuchunguza ili mtuhumiwa (Dk. Amita) apate haki ya kusikilizwa.

Hata hivyo, mwajiri ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni alipopata taarifa kwamba Tume ya Utumishi wa Umma haikuridhia uamuzi wake wa kumsimamisha kazi mtumishi huyo, alikata rufani kwa rais.

"Nilikuwa ninajaribu kujiuliza wakati nimeunda kamati ya kunishauri jambo hili, nikauliza madaktari wa upasuaji ukishakuwa kwenye jopo kwamba huyu mgonjwa afanyiwe operesheni, wewe unayekwenda kumfanyia una haki zipi? Wakasema unaweza kwenda kwenye chumba cha operesheni na ukaamua kuahirisha kutokana na hali ya mwisho ya mgonjwa," alisema.

Simbachawene alisema katika sakata hilo, hakuna aliyemsaidia Dk. Amita (mtuhumiwa) na badala yake mwajiri akaona kukata rufani ndiyo njia mwafaka na kusababisha lichukue muda mrefu kutokana na kuwapo mvutano kati ya mkurugenzi na Dk. Amita.

Alisema kuwa kwenye ngazi za mikoa na mamlaka za serikali za mitaa, watumishi wanaonewa sana, jambo ambalo serikali haipendi kuona linaendelea.



Mkurugenzi Mtendaji wa Crystal Human Capital, Kabeho Solo (kushoto), akikabidhi msaada wa vitabu vya elimu ya biashara kwa Kaimu Amidi wa Shule Kuu ya Biashara ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDBS), Dk. Patrick Mbwile chuoni hapo, jana. Kulia ni Mkurugenzi wa Wealth Capital Fund, Paul Mashauri. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# 'Masharti kuasili watoto ni magumu'

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MBUNGE wa Viti Maalum (CHADEMA), Hawa Mwaifunga, ameitaka serikali kufanya marekebisho ya sheria za kuasili watoto kwa kuwa imekuwa ngumu, hata kusababisha watu washindwe kuasili watoto na kuchangia ongezeko la watoto mitaani.

Akiuliza swali la nyongeza bungeni jana, mbunge huyo alihoji kama serikali haioni jambo hilo linahitaji kurahisishwa ili kuwasaidia watoto hao walioko mitaani.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Mwanaidi Ali Khamis, alisema serikali inawajali watoto katika malezi na makuzi na inavyo vituo viwili vya kulelea watoto Kikombo na Kurasini na vya binafsi.

Alisema wale wote wenye changamoto na watoto za kulelewa, wafike ofisi za ustawi kwa kuwa sheria na miongozo ipo. Watapata haki zao za msingi.

Katika swali la msingi, mbunge huyo alihoji lini serikali italeta mabadiliko ya sheria ya kuasili watoto kwa kuwa iliyopo imepitwa na wakati.

Naibu Waziri huyo, akijibu swali hilo, alisema kuwa mwaka jana serikali imefanya mabadiliko ya Sheria ya Ulinzi wa Mtoto kuhusu masuala ya uasili wa mtoto kwa kuboresha mifumo na kuimarisha taratibu za kuasili nchini.

Alisema mabadiliko hayo yalipitishwa na Bunge na kusisitiza kuwa serikali itaendelea kufanya mapitio ya sera na sheria mbalimbali kwa kadri itakavyohitajika kwa lengo la kuimarisha ulinzi na ustawi wa mtoto.

# TLP yapata mrithi wa Mrema, 21 wafukuzwa uanachama

**Na Elizabeth Zaya**

CHAMA cha Tanzania Labour Party (TLP) kimemchagua Richard Lyimo kuwa mwenyekiti mpya wa chama hicho atakayeongoza kwa miaka mitano ijayo huku wanachama 21 wakifukuzwa uanachama.

Tangu kufariki dunia Agustino Mrema mwaka 2022, nafasi hiyo ilikuwa inakaimiwa na Hamad Mkadamu. Lyimo alichaguliwa katika Mkutano Mkuu wa Chama hicho uliofanyika mwishoni mwa wiki mkoani Dar es Salaam, ukihudhuriwa na wajumbe 84.

Katika uchaguzi huo, Lyimo alikuwa mgombea pekee katika nafasi hiyo ya mwenyekiti na kabla ya kuchaguliwa katika nafasi hiyo, alikuwa Katibu Mkuu wa TLP. Wajumbe wa mkutano huo walimchagua Johari Hamis kuwa Makamu Mwenyekiti Bara. Alikuwa mgombea pekee.

Mkutano huo kwa kauli moja uliridhia kuwafuta uanachama, wanachama 21 wa chama hicho, wakiwamo viongozi wanaodaiwa kufanya majaribio ya kuandaa mikutano miwili ya kuchaguana kinyume cha katiba ya chama chao. Walitaka kujaza nafasi iliyokuwa imeachwa wazi na Mrema.

Miongoni mwa wanachama na viongozi waliofukuzwa ni Dominata Rwechangura aliyekuwa Makamu Mwenyekiti Bara, Ivan Maganza aliyekuwa Mwenyekiti wa Vijana Taifa na Mariam Kassin.

Wengine waliofukuzwa ni Riziki Nganga, Stanley Ndumagoba, Mary Mwaipopo, Mohamed Mwinyi, Laurian Kazimiri, Nataria Shirima, Kinanzaro Mwanga, Godfrey Stivin na Rashid Amiri. Pia wamo Twaha Hassan, Tunu Kizigo, Damari Richard, Hamad Alawi, Mohamed Hemed, Mariam Hamis, Mussa Fundi, Mwajuma Mussa na Osward Nyoni.

Naibu Msajili wa Vyama vya Siasa, Sisty Nyahoza alithibitisha mkutano huo uliomchagua Lyimo na wenzake pamoja na kuwafukuza baadhi ya wanachama hao ulifanyika kihalali. Aliwataka wenye malalamiko kuhusiana na chochote kilichofanyika katika mkutano huo, wampelekee malalamiko yao.

"Mkutano ulifanyika kihalali na aliyepitishwa anatambuliwa kikatiba na taratibu za chama chao na walishatoa taarifa, kwa hiyo yote yaliyofanyika ni halali na yana baraka kutoka kwa wajumbe wa mkutano, wenye malalamiko waniletee kwa kufuata utaratibu, nitayashughulikia," alisema Nyahoza.



# Mahakama yaomba upya orodha mali za marehemu

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

MAHAKAMA Kuu, Kanda ya Moshi imeamuru msimamizi wa mirathi ya mfanyabiashara maarufu mjini Moshi marehemu, Paul Njau, aliyefariki mwaka 2002, kupeleka upya orodha ya mali za marehemu, baada ya kubaini mgawanyo wa mali haukufuata taratibu.

Kumbukumbu zinaonyesha kuwa msimamizi wa mirathi, Emmanuel Kyauka Njau hakuwa amegawa mali kwa usawa.

Amri hiyo imo katika maelekezo ya Jaji Safina Semfukwe, anayesikiliza shauri hilo la mirathi lililofunguliwa na baadhi ya ndugu wakiongozwa na Catherine Kyauka.

Baadhi ya ndugu wanalalamikia mgawanyo wa mali na kutofungwa kwa mirathi ya marehemu baba yao.

Jaji, alimtaka msimamizi huyo kwenda kukaa na wakili wake pamoja na ndugu zake na kuandaa upya orodha ya mali za marehemu na kuiwasilisha mara moja mahakamani.

"Haiwezekani msimamizi wa mirathi ukawa huna nyaraka zinazoonesha orodha ya mali za marehemu ulizodai umegawa , nakuagiza kakae na ndugu zako pamoja na wakili wako muandae upya 'Inventory' na kuiwakilisha mahakamani siku ya Alhamisi (Februali 6) ili ndugu waipitie na kesi ya msingi ianze kusikilizwa siku ya Jumatatu (Februari 10), " alisisitiza.

Adha, alikataa ombi la msimamizi huyo wa mirathi la kutaka kuondoka na kurejea nchini Uingereza kwa madai ya kuwahi majukumu yake ya kazi.

Hivyo, alimtaka kukamilisha kwanza jambo hilo la kuorodhesha mali za marehemu kwani kesi hiyo imedumu kwa miaka 23 tangu (Paul) alipofariki dunia Feb, 17 mwaka 2002 na akiondoka atakuwa amejikosesha haki yake ya kusikilizwa.

"Tulichobaini hapa inventory haikuwahi kufailiwa kilichokuwa kimefailiwa hapa ni valuation hivyo natoa amri kwa msimamizi wa mirathi nenda ukatuletee inventory mpya," alisema.

Pia Jaji Semfukwe aligoma kuahirishwa kesi hiyo na kuisogeza hadi Juni mwaka huu kama alivyoiomba msimamizi wa mirathi ili aweze kujiandaa vizuri.

Baadhi ya ndugu waliofika mahakamani akiwemo Richard Kyauka Njau, aliishukuru mahakama kwa uamuzi wa kumzuia msimamizi wa mirathi asiondoke nchini mpaka ahakikishe amekamikisha kuandaa orodha ya mali za marehemu kwani imekuwa vigumu kumpata.

Awali kabla ya kusikilizwa kwa shauri hilo, Jaji Semfukwe aliagiza kuitwa kwa msimamizi huyo wa mirathi aliyekuwa Uingereza baada ya kukosekana kwa nyaraka muhimu ikiwamo orodha ya mali za marehemu. Kesi hiyo imepangwa kusikilizwa Februari 10, mwaka huu.

# Gwajima: Siku ya Wanawake kutathmini hatua, mafanikio katika ujenzi wa taifa

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Doroth Gwajima, amesema maadhimisho ya Siku ya Wanawake Kitaifa yatakayofanyika mkoani Arusha, Machi 8 mwaka huu, yatakuwa mahsusi kwa ajili ya kutathmini hatua iliyofikiwa na wanawake katika ujenzi wa taifa.

Amesema maadhimisho hayo yatafanyika mkoani Arusha kwa sababu mkoa huo unamatukio mengi kandamizi ya mila, desturi dhidi ya wanawake.

Akizungumza na waandishi wa habari, Dk. Gwajima alisema licha ya matukio ya ukatili wa kijinsia kushuka nchini kutoka asilimia 10 mwaka 2016 hadi nane mwaka 2023 mikoa ya Arusha na Manyara bado inaongoza kwa matukio ya ukatili wa kijinsia.

Dk. Gwajima alisema kauli mbiu ya mwaka huu inasema; 'Wanawake na wasichana 2025 tuimarishe haki, usawa na uwezeshaji' kwamba inalenga kuhamasisha wanawake wajitokeze kushiriki nafasi za uongozi katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka huu.

Wakati Dk. Gwajima akieleza hayo, Mkoa wa Arusha umeanza maandalizi, huku Mkurugenzi Mtendaji wa Jiji hilo, John Kayombo, akidokeza kuchinjwa ng'ombe 50 kwa ajili ya kusherehesha maadhimisho hayo.

"Huko mitaani kuna wanawake wanafanya vizuri, tukawaibue wajulikane na hata kufahamu changamoto zao kupitia jukwaa la maadhimisho ya Siku ya Wanawake Kitaifa yatakayofanyika Arusha," alisema Gwajima.

Maadhimisho hayo ni fursa ya kuwakutanisha wadau mbalimbali wa uwezeshaji wanawake kujadili hatua zilizofikiwa katika utekelezaji wa mikakati ya kuwainua.

Mkurugenzi Mtendaji wa Jiji la Arusha, John Kayombo, amewasihi wananchi wajipange kwa ajili ya shughuli hizo, ambazo zitakuwa na matukio mbalimbali kwa takribani siku nne.

Kwa mujibu wa Kayombo, huduma mbalimbali zitatolewa ikiwamo huduma ya matibabu kwa wagonjwa wasiojiweza.

Alisema maadhimisho ya Siku ya Wanawake Kitaifa yatafanyika kwa utofauti na miaka mingine, ambapo kwa mwaka huu yatahusisha shughuli za siku nne, yakiwamo maonyesho ya biashara za wanawake, michuano ya mpira wanawake na burudani mbalimbali.



Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Mkoa wa Tanga, Rajabu Abdulrahman (wa tatu kushoto), akikagua utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa madarasa, mabweni na matundu ya vyoo, katika Shule ya Sekondari Makose, Kata ya Malindi, Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto, mwishoni mwa wiki, akiwa katika ziara yake kuelekea maadhimisho ya Miaka 48 ya chama hicho. Wa tatu kulia ni Mkuu wa Wilaya ya Lushoto, Zephania Sumaye. **PICHA: ASHRACK MIRAJI**

# Wajengewa daraja baada ya miaka 64

**Na Godfrey Mushi,** HAI

MFANYABIASHARA na mdau wa maendeleo wa Wilaya ya Hai, mkoani Kilimanjaro, Shaaban Mwanga, amemaliza changamoto ya miaka 64 ya ukosefu wa daraja dogo la Kibohehe katika Kata ya Machame Romu.

Waathirika wakuu waliokumbana na adha ya kukosekana kwa kivuko hicho ni wananchi, waendesha pikipiki na wanafunzi wa shule za msingi Roo, Kibohehe, Tolu na Shule ya Sekondari Kibohehe.

Akizungumza na waandishi wa habari alipokwenda kuzindua daraja hilo dogo lililogharimu zaidi ya Sh. milioni 4.15, Mwanga, alisema eneo hilo ambalo limeinuka mara nyingi wakati wa mvua wananchi hupata adha kubwa ya kuvuka upande wa pili kwenda upande mwingine.

Alisema kabla ya ujenzi wa daraja hilo dogo wananchi walikuwa wakitumia gharama kubwa za usafiri, usafirishaji wa mazao yao kutoka shambani na majumbani kwenda katika Soko la Kimataifa la Mazao la Kwa Sadala.

"Kubwa lililotukutanisha hapa ni uzinduzi wa daraja letu (kivuko), ambalo baada ya kuanza ujenzi wake Oktoba 06 mwaka jana. Eneo hili limekuwa ni korofi kama mnavyoona.

"Sio wananchi wa kawaida tu, hata waendesha pikipiki kwa maana ya bodaboda na wanafunzi, wakati wa mvua kubwa mawasiliano yanakatika kutoka eneo moja kwenda jingine na hawawezi kuendelea na safari.


...Wananchi walikaa wakaona kwamba iko haja kunishirikisha mimi kama mdau wa maendeleo, tukakaa nao tukaangalia ni jinsi gani kusaidiana kujenga hilo daraja," alisema.

Akisoma risala ya wananchi wa Kibohehe, David Shuma, alisema mradi huo wa ujenzi wa daraja dogo umetumia Sh. milioni 4.15, huku deni linalotokana na gharama za ujenzi likiwa Sh. 564,000.

Kutokana na deni hilo, mfanyabiashara huyo Shabaan Mwanga, ameahidi kulilipa, kwa sharti la wananchi nao kuchangia Sh. 64,000.

Mmoja wa wakazi wa Kibohehe na Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM, Wilaya ya Hai, Sadaat Kweka, alisema wanaoujua ukweli na machungu ya kukosekana kwa kivuko hicho, tangu kupatikana kwa uhuru ni wananchi wa Kibohehe.

Alisema: "Hiki kivuko (daraja dogo) katika korongo la Kibohehe, limepunguza utoro kwa wanafunzi wa shule za msingi Roo, Kibohehe, Tolu na Shule ya Sekondari Kibohehe".





# Wachimbaji wahofiwa kufia mgodini

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WACHIMBAJI wadogo watatu katika mgodi wa dhahabu wa Nkandi uliopo mtaa wa Ilindi-Mwime Kata ya Zongomela Manispaa ya Kahama, wanahofiwa kufariki dunia baada ya kufukiwa na kifusi cha udongo katika duara walilokuwa wakichimba madini.

Tukio hilo limetokea Februari Mosi, mwaka huu majira ya saa nne asubuhi wakati wachimbaji hao wakiendelea na shughuli za uchimbaji wa madini.

Baadhi ya mashuhuda wa tukio hilo akiwamo Meneja wa Mgodi huo, Mdaki Shabani, alisema mpaka kufikia Februari 2 jioni wachimbaji hao walikuwa hawajaokolewa kutokana na maduara hayo kujaa maji kutokana na mvua inayoendelea kunyesha.

Aidha, alisema chanzo cha duara hilo kumeguka na kuwafunika wachimbaji ni ukosefu wa umeme kwa muda wa wiki mbili na kuchelewesha uondoaji wa maji ndani ya maduara hayo.

Alisema walitoa taarifa kwa Meneja wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) na mpaka sasa hakuna jitahida zilizofanyika.

Shabani alisema, wameshindwa kuwaokoa kwa wakati kutokana na duara kuwa limejaa maji mengi na kuwa wanaendelea kuondosha maji ili kupata njia ya kuingia na kuwatoa.

"Umeme ungekuwapo tungekuwa tayari tumewaondoa tangu Februari Mosi kwasababu maji hayo yanatolewa kwa kuvutwa kupitia mashine za umeme," alisema Shabani.

Mchimbaji na mwokoaji katika tukio hilo, Joseph Marco aliyezama ndani ya duara alieleza hali ya maji ndani ya duara kuwa ni mbaya kwani maji ni mengi na hivyo kuwapa changamoto ya kuwafikia na kushauri kuangalia namna ya kuyaondoa ili kupata njia ya kuwafikia.

Hata hivyo, aliwaomba wamiliki wa leseni na msimamizi wa duara hilo kuhakikisha wachimbaji wanaoingia duarani wanakuwa na vifaa kinga vinavyotakiwa kwa ajili ya usalama wao.

"Kunagema la udongo lilishuka likaziba njia na tukiyaondoa au kuyapunguza maji yaliyopo duarani tutafanya utaratibu wa kuitoa miti iliyokuwa imelishikilia na kuwatoa ndugu zetu, tunatakiwa kuongeza kasi ya ukoaji ili tuweze kuwasaidia," alisisitiza Marco.

Akithibitisha kutokea kwa tukio hilo, Mkuu wa Zimamoto na Ukoaji Wilaya ya Kahama, Mkaguzi Msaidizi, Hafidhi Omary alisema juhudi za ukoaji zinaendelea na kuwa mpaka sasa hawajawafikia kwasababu ya duara kuwa na maji mengi.

Aidha, alisema uokoaji unaendelea kwa kushirikiana na wachimbaji na kwamba wameshindwa kuendelea na shughuli za uokoaji na badala yake kuanza kutoa maji ndipo waweze kuendelea na ndiyo sababu inayowachukulia muda.



Mkuu wa Wilaya ya Ilemela, Hassan Masala (wa pili kushoto), akiongozana na wakazi wa Mtaa wa Buyobe, Kata ya Kahama juzi, kufanya uhakiki wa eneo linalodaiwa kuwa na mgogoro baina ya wananchi na Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), unaodaiwa kuuza maeneo yao bila kuwalipa fidia. **PICHA: VITUS AUDAX**

# Waomba kumalizwa mgogoro wa ardhi uliodumu miaka 19

**Na Vitus Audax,** MWANZA

WAKAZI wa Mtaa wa Buyombe Manispaa ya Ilemela mkoani Mwanza wameiomba serikali kumaliza mgogoro wa ardhi uliodumu kwa zaidi ya miaka 19 kati yao na Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF).

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti baadhi ya wananchi hao akiwamo, Suleiman Sabuli alisema mgogoro huo ulianza baada ya halmashauri kuuza viwanja vyao kwa NSSF bila wao kupata fidia.

"Juzi tumeletewa barua na NSSF tunaambiwa kuwa watu wote wa Buyombe tulivamia maeneo yao, kwa hiyo wanatutaka kila mmoja tununue tena kiwanja katika eneo lake kwa kila mita ya mraba moja Sh.15,000," alisema Sabuli.

Sabuli aliongeza: "Sasa maajabu ni kwamba mimi eneo ni langu na sijalipwa fidia halafu tena uniuzie wewe, sasa hii ni kwa maana gani?... Tunamwomba Rais Samia Suluhu Hassan atusaidie katika suala hili."

Mkazi mwingine wa mtaa huo, Rehema Idd alisema kwa sasa ombi lao ni kwa serikali pamoja na Rais Samia kulitazama suala hilo kwani limekuwa likiwazuia kufanya shughuli za maendeleo.

"Tumeteseka vya kutosha, tumezuiliwa kumalizia nyumba zetu, mbao zinapinda, saruji zinaganda kisa ni kutii na kufuata sheria ya zuio tulilopewa," alisema mkazi huyo.

Akijibu madai hayo Meneja Miliki wa NSSF Mkoa wa Mwanza, Jofrey Timothy alisema mfuko huo una maeneo nchi nzima na kwamba kitendo cha kuruhusu watu kuvamia maeneo yake kinaruhusu wakazi wa maeneo mengine kufanya hivyo.

Baada ya kilio hicho, Mkuu wa Wilaya ya Ilemela, Hassan Masala, alifika katika eneo hilo na kutumia muda wa zaidi ya saa tatu kuzungukia maeneo yote ya mtaa huo yanayotajwa kuwa katika mgogoro wa kutokulipwa fidia.

"Awali nilifika hapa na kutoa maelekezo lakini baada ya maelekezo hayo kuna vitu ambavyo baadhi ya wananchi hawakuridhika navyo, hivyo ikanibidi nirudi kufanya ukaguzi na kupita eneo kwa eneo ili kubaini tatizo lilipo," alisema Masala.

Aliongeza: "Baada ya kuunda timu tumebaini nyumba 175 zimejengwa katika maeneo yaliyonunuliwa na NSSF pamoja na mwendelezo mpya wa nyumba 22, huku viwanja 230 vikiwa bado havijaguswa kabisa. Tumekubaliana viwanja ambavyo havijaguswa viendelee kuwa mali ya NSSF na hivi vilivyojengwa tunaweka utaratibu mzuri kati ya wananchi na NSSF".

Alisema baada ya maelekezo hayo baadhi ya wananchi walionesha kutokuridhika, hivyo kumlazimu (DC) kurudi na kuzunguka maeneo yote kufanya uhakiki, kuahidi kurejea tena wiki hii kutoa uamuzi wa mwisho juu ya mgogoro huo baada ya uchunguzi kukamilika.

## RC atangaza 'vita' dhidi wanaochunga mifugo mjini

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MKUU wa Mkoa wa Shinyanga, Anamringi Macha, amewaagiza wakuu wa wilaya na wakurugenzi, kuwachukulia hatua wafugaji wa maeneo ya mjini, ambao wamekuwa wakichunga mifugo yao kiholela na kuharibu miti.

Alitoa agizo hilo juzi wakati wa kupanda miti 500 katika Shule ya Msingi Mapinduzi ikiwa ni sehemu ya kutekeleza kampeni ya utunzaji wa mazingira katika kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi.

"Miti hii 500 ambayo tumeipanda naagiza itunzwe vizuri pia kwa wananchi, taasisi na halmashauri zote sita za mkoa endeleeni kupanda zaidi katika maeneo yenu, pamoja na maeneo ya machimbo ya madini ili kuifanya Shinyanga ya kijani," alisema Macha.

Katika hatua nyingine Macha alimpongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa utendaji wake mzuri, akitaja mchango wake katika uongozi wa kimataifa hata kuongoza mkutano wa nishati.

Alisema masuala ya nishati yanasaidia pia katika matumizi ya nishati safi ya kupikia na kuondokana na utegemezi wa mkaa na kuni ambazo husababisha uharibifu wa mazingira kwa kukata miti ovyo.

Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Julius Mtatiro, alisema maelekezo yote ambayo yametolewa na Mkuu wa Mkoa watayafanyia kazi pamoja na kuendelea kutekeleza maagizo ya kampeni ya kupanda miti.

Meya wa Manispaa ya Shinyanga, Elias Masumbuko, alisema wataifuatilia miti hiyo 500 ambayo imepandwa katika shule hiyo pamoja na kuhamasisha jamii kupanda miti na kuifanya shinyanga kuwa ya kijani.


Mmoja wa wanafunzi wa shule hiyo, Godfrey Mgeta, alisema wao kushiriki katika upandaji miti kumewasaidia kuelewa umuhimu wa miti na watakuwa mabalozi wazuri wa kuhamasisha upandaji miti majumbani kwao.



Ukurasa 12

**Mradi mageuzi ya usawa kijinsia kwenye elimu unapoanzia Tanga**






Ukurasa 13

**MATOKEO IV ZANZIBAR:**

**Lazima kuchukua hatua haraka kuimarisha elimu**

Nipashe

# TESA

Jumanne Februari 4, 2025

TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI

ELIMU

NA SABATO KASIKA

# Ni msako nyumba kwa nyumba kufikisha wenye ulemavu darasani

KUWATUMIA watu wanaoishi na ulemavu ili kujinufaisha mfano kuwaweka barabarani na bakuli kuomba fedha ni mambo yanayofanyika kwenye miji na majiji mengi.

Inasikitisha kuona wengine wanaungua jua kutwa na baadhi wakinyeshewa na mvua, wakishinda kutwa wamelowana ili mradi wamewekwa kuwatafutia jamaa zao mapato.

Pamoja na kutumiwa kuomba fedha barabarani, zipo familia zinazowaficha ndani wakiwaona kuwa ni mkosi, bila kujua kuwa watoto hao wana mchango wa maendeleo kama watapewa maarifa na vipaji vyao kuendelezwa.

Baadhi ya wadau wa watetezi haki za watoto likiwamo Shirika la Kaya Foundation, limeanza kupunguza ukubwa wa tatizo la wenye ulemavu kukosa elimu na huduma muhimu, likiwasaka na kuwafikisha shuleni.

Kaya imejikita kuwasaka nyumba hadi nyumba na kuwapeleka shuleni kwenye maeneo likifanya kazi hiyo Chamazi, Vingunguti, Segerea na Kinyerezi jijini Dar es Salaam.

Aidha, linawahudumia pia wanawake 20 wenye ulemavu, anasema Annapili Ngome, Mkurugenzi wa Kaya Foundation.

Katika mazungumzo na gazeti hili wakati wa kilele cha maadhimisho ya Siku ya Elimu Duniani jijini Dar es Salaam, Annapili, anasema licha ya jitihada mbalimbali za serikali na wadau kutaka watoto wenye ulemavu wapate elimu, bado kuna kukwama.



Baadhi ya watoto wanaohudumiwa na Kaya Foundation. **PICHA: SABATO KASIKA**

Matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi iliyofanyika 2022 yanataja idadi ya watu wanaoishi na ulemavu kuwa ni milioni 5.34 karibu sawa na asilimia 11.2 ya Watanzania.

Annapili anataja baadhi ya wazazi walezi wanaowaficha majumbani na kuwakosesha fursa ya kusoma kuwa ni kikwazo.

"Shirika letu linajishughulisha na watoto wenye ulemavu na mahitaji maalum, lilianzishwa mwaka 2023 kwa lengo la kuibua watoto hao kutoka majumbani na kuwapeleka shuleni. Tumekuwa tukishuhudia hali hiyo katika baadhi ya familia," anaongeza.

Akielezea jinsi anavyofanya kazi, anasema huwatembelea wananchi wakianzia kwenye ofisi za serikali za mitaa mbalimbali kuelezea lengo lake ili kujua idadi ya watoto aina hiyo katika mtaa ambao hawapelekwi shule.

"Kwa njia hiyo tumepata watoto 35 wanaoshi na wazazi na walezi , 15 kati yao sasa wanasoma katika shule mbalimbali za msingi za umma wilayani Temeke na Ilala, na tisa kati yao walianza darasa la kwanza mwaka huu," anasema.

Mkurugenzi huyo anafafanua kuwa wanachokifanya ni kufika katika nyumba zenye watoto walemavu na kutoa elimu kwa wazazi au walezi kuhusu haki za watoto hao ikiwamo kupata elimu.

Anasema mlemavu ana haki zote ikiwamo ya kusoma, kulindwa, kutunzwa na kupewa matibabu, kuishi, kuheshimiwa na kutokubaguliwa, kupewa jina, utaifa na kuwafahamu wazazi wake, kutoa mawazo na maoni, kuepushwa na mateso na udhalilishaji na kurithi mali za wazazi wao wapofariki.

"Kwa miaka miwili tunajishughulika na watoto wenye ulemavu na mahitaji maalum, hivyo tuna uzoefu na kile ninachokieleza hasa vitendo vya kuwaficha, kutojua haki zao na kuwatenga," anasema.

Hata hivyo, anasema wapo baadhi ya wazazi na walezi ambao hupeleka watoto hao shule na kukataliwa, na kwamba shirika hilo linawaelekeza njia ya kufanya ikiwa ni pamoja na kujua kuwa kuna elimu jumuishi.

"Elimu jumuishi inahusisha watoto wasio na ulemavu na wenye ulemavu, hivyo wanapokutana na changamoto ya kukataliwa, tunaingilia kati kuhakikisha wanapokelewa katika shule za umma," anasema.

Mkurugenzi huyo anasema, kwa kuwa shirika lake linatoa pia msaada wa kisheria kwa watoto na wanawake na makundi mengine yaliyotengwa kwenye jamii linahakikisha watoto wenye ulemavu wanapata haki zao.

Anasema ingawa bado wapo wazazi na walezi wanaowaficha watoto wao wenye ulemavu, wanajitahidi kuwaelimisha watambue kuwa watoto wenye ulemavu wana haki kama wengine wenye viungo kamili.

**INAENDELEA UK.14**

ELIMU

NA ELIZABETH ZAYA,
ALIYEKUWA TANGA

# Mradi mageuzi ya usawa kijinsia kwenye elimu unapoanzia Tanga

KUKOSA ufahamu wa masuala ya usawa kijinsia na uhaba wa miundombinu muhimu shuleni ni miongoni mwa vichocheo vinavyowarudisha nyuma wasichana na kukwamisha maendeleo yao kielimu.

Ili kufikia usawa wa kijinsia kwenye elimu, wadau wameanzisha mkakati wa kuboresha miundombinu ya maji, usafi wa mazingira, kuondoa ukatili wa kingono na kijinsia shuleni ili wasichana wasikatishe masomo.

Taasisi ya HakiElimu imezindua mradi wa Mageuzi ya Usawa wa Kijinsia katika Elimu (MMUKE), mkoani Tanga utakaofikia shule za msingi 16 na za sekondari 24 za mikoa minane ya Bara kwa gharama ya Sh.bilioni 7.8, ikishirikiana na Serikali ya Canada.

Akizungumza wakati wa uzinduzi huo, Mkurugenzi wa HakiElimu, Dk.John Kalage, anasema lengo ni kuwekeza vifaa vya maji, usafi wa mazingira na wa mtu binafsi ili kufanikisha jitihada za wasichana kuendelea na masomo.

Anasema wanaotarajiwa kufikiwa ni wasichana 12,240 na wavulana 11,760 wenye miaka 10 hadi 19, walengwa wakuu kwenye wa mradi huo utakaofanyika kwa miaka minne.

Kwenye maji, anasema shule nyingi hazina vyanzo vya maji na mifumo ya uhakika, vifaa vya usafi wa mazingira na wa mtu binafsi.

"Kwa ushirikiano wa jamii, HakiElimu inaboresha mifumo hii ikizingatia mahitaji ya kijinsia kwenye shule 40 za mradi, kwa manufaa ya wanafunzi 24,000 wavulana na wasichana. Tunawekeza katika ujenzi wa visima vya maji na kujenga vyoo vya wasichana vilivyo na vyumba maalumu vya kubadilishia taulo na kujisitiri wakati wa hedhi," anasema Dk.Kalage.

"Pia HakiElimu, tunaendesha mafunzo na kutoa elimu ya umuhimu na matumizi sahihi ya miundombinu ya usafi inayozingatia mahitaji ya kijinsia katika jamii za shule ikiwamo walimu, wanafunzi na wazazi."

Dk.Kalage anasema lengo la kufanya hivyo ni ili kuwapo na ushiriki wa jamii yote na kwamba katika kufanikisha hili pia inawezesha vikao vya majadiliano katika jamii hiyo kwa lengo la kuhamasisha watu wa maeneo husika kuhusu usafi wa mazingira na usafi binafsi unaozingatia mahitaji ya kijinsia.




Mkuu wa Wilaya ya Korogwe, William Mwakilema (mwenye tai) na Mkuu wa Shirika la Maendeleo la Canada, Carol Mundle (kulia), wakizindua mradi wa mageuzi ya usawa kijinsia. **PICHA: ELIZABETH ZAYA**

> Kwa ushirikiano wa jamii, HakiElimu inaboresha mifumo hii ikizingatia mahitaji ya kijinsia kwenye shule 40 za mradi, kwa manufaa ya wanafunzi 24,000 wavulana na wasichana.

Jambo jingine ambalo anasema mradi huo utazingatia ni pamoja na kuimarisha klabu za jinsia kwa ajili ya kuwajengea uwezo wasichana walio katika umri wa kijalunga.

Kupitia klabu hizo, uelewa miongoni mwa wavulana na wasichana kuhusu haki zao sawa na usawa wa kijinsia utaongezeka na kuwa jukwaa la kuwaelimisha vijana kuhusu afya ya uzazi, hedhi na ukatili dhidi ya watoto.

Anasema klabu hizo zitakuwa na kazi ya kuhakikisha kwamba wasichana wanajua jinsi ya kujilinda na kwamba pia kutakuwapo na mafunzo ya kujenga uwezo kwa makundi hayo ambayo yatafanyika kwa ushirikiano na wauguzi wa eneo husika pamoja na dawati la jinsia la Jeshi la Polisi.

"Zaidi ya hayo, unalenga kuimarisha uwezo wa waangalizi wa wanafunzi shuleni (matroni) na walimu ili waendelee kutoa mwongozo kwa klabu za jinsia kuhusu mada kama za afya ya uzazi, namna ya kufanya maamuzi, haki za wasichana, shinikizo la rika, mipango ya maisha ya baadaye na mwongozo wa taaluma," anasema Dk.Kalage.

"Tunaamini mambo yote haya yatawajenga wasichana kujiamini na kuwawezesha kufanya maamuzi sahihi. Kwa hiyo wasichana wa klabu za jinsia, wanahimizwa kutumia mbinu ya rika katika kujifunza, kushirikiana walichojifunza na vijana wengine kupitia mikutano iliyoandaliwa, ziara za kielimu, matukio mbalimbali pamoja na shughuli zinazojumuisha michezo na maigizo."

Anasema kupitia mradi huo, HakiElimu inandaa kampeni za kujenga uelewa wa jamii kwa ajili ya kuongeza ufahamu wa jamii zinazozunguka shule kuhusu madhara na athari za ukatili wa kijinsia na kingono shuleni kupitia sanaa za maonesho ya jukwaani, ujumbe mfupi wa maandishi, ujumbe wa sauti na vipindi vya redio za kijamii.

Katika kuimarisha mbinu za kuzuia ukatili dhidi ya watoto katika shule za mradi, Dk.Kalage anasema shule zote zinazoshiriki zinakuwa na mifumo inayofanya kazi ya kuzuia ukatili huo wa kijinsia na kingono na ukatili dhidi ya watoto.

"Hii inajumuisha usimikaji, wa masanduku ya kutoa taarifa yanayoitwa 'sauti yangu' katika maeneo yanayofikika kwa urahisi ndani ya shule. Masanduku haya hufungwa kwa usalama na hufunguliwa kila wiki na timu ya marafiki wa elimu, matroni patroni na angalau wasichana wawili wa vilabu vya jinsia.

"Kwa pamoja wanapitia taarifa wanakubaliana hatua zinazotakiwa kuchukuliwa na kufuatilia maendeleo ya utekelezaji, iwapo tukio la unyanyasaji linaripotiwa mamlaka husika hujulishwa mara moja kwa hatua zaidi, tunatambua kazi inayofanywa na marafiki wa elimu katika kufuatilia mara kwa mara kesi zinazoripotiwa," anasema Dk.Kalage.

Anasema katika kufanikisha kazi ya kupambana na vitendo vya ukatili, wamekuwa wakishirikiana kwa karibu na vyombo vya usalama pamoja na mashirika mengine katika kuhakikisha kwamba kesi za watoto dhidi ya ukatili zinashughulikiwa ipasavyo na kufikia tamati kwa kupata suluhisho stahiki.

Anasema wanaunga mkono ujenzi na ukarabati wa hosteli za wasichana katika shule zilizochaguliwa ili kupunguza changamoto ya kutembea umbali mrefu na kuhakikisha wasichana wanakuwa katika mazingira salama.

Katika ngazi za wilaya anasema utatekelezwa wilayani Mkuranga mkoani Pwani, Kilosa Morogoro, Mpwapwa Dodoma, na Babati mkoani Manyara.

Dk Kalaghe anazitaja wilaya nyingine kuwa ni Iramba mkoani Singida, Muleba Kagera, Musoma Mara na Korogwe mkoani Tanga.

Kadhalika, aansema utawafikia wanajamii 140 na maofisa 320 wa mamlaka za serikali za mitaa kupitia mijadala ya kijamii na mafunzo ya kujenga uwezo yenye lengo la kuongeza uelewa kuhusu kuzuia ukatili wa kijinsia na umuhimu wa kukuza usawa wa kijinsia katika elimu.

Mkuu wa Shirika la Maendeleo la Canada, Carol Mundle, anasema wanajivunia kuwa sehemu ya mafanikio ya uanzishwaji wa mradi huona kwamba wanaamini mradi huo utasaidia kongeza ufaulu wa wanafunzi katika maeneo unakotekelezwa.

Anaipongeza Tanzania kufikia usawa wa kijinsia kwenye maeneo ya kuandikisha wanafunzi shuleni na kuwahimiza wazazi na walimu kushirikiana na HakiElimu kwa sababu na wao ni sehemu ya uendeshaji wa mradi huo.

Mkuu wa Wilaya Korogwe, William Mwakilema, anasema wataendelea kutoa ushirikiano kupitia mradi huo ili kufanikisha utekelezaji na upatikanaji wa matokeo yaliyokusudiwa.

Anasema ni muhimu kwa wananchi na halmashauri hiyo kuuelewa na kuendelea kufuatilia na kutoa ushirikano katika maeneo unakotekelezwa.

ELIMU
NA KHALED GWIJI

MATOKEO IV ZANZIBAR:
# Lazima kuchukua hatua haraka kuimarisha elimu

MATOKEO ya mtihani wa kidato cha nne Zanzibar yanaashiria changamoto kubwa na ya dharura katika mfumo wa elimu, ambayo haipaswi kupuuzwa.

Hali hii inapaswa kutazamwa kama janga la kitaifa linalohitaji juhudi za pamoja kutoka kwa viongozi wa kisiasa, walimu, wazazi, walezi na jamii nzima.

Takwimu zilizopo zinathibitisha kuwa hata skuli au shule zilizoongoza Zanzibar hazikuweza kushindana ipasavyo katika ngazi ya shule za Muungano.

Kwa mfano, Shule ya Fidel Castro, ambayo ni ya kwanza Zanzibar, imekuwa nafasi ya 26 ndani ya Muungano, huku nyingine nyingi za Zanzibar zikiwa nafasi za chini ya 200.

Tofauti hii inaonyesha hitaji kubwa la mageuzi ya haraka ili kuboresha ubora wa elimu Zanzibar.

### CHANZO CHA TATIZO

Changamoto za elimu Zanzibar zinaweza kufungamanishwa na mambo yafuatayo, ubora wa walimu na mafunzo, walimu wengi hawapati mafunzo ya mara kwa mara yanayolenga kuboresha mbinu za kisasa za ufundishaji.

Nyingine ni mishahara duni na mazingira magumu ya kazi yanadhoofisha ari na motisha ya walimu.

Miundombinu duni, wakati shule au skuli nyingi zinakabiliwa na changamoto ya ukosefu wa madarasa ya kutosha, maabara za kisasa, maktaba bora, na vifaa vya kufundishia, ni changamoto nyingine.

Baadhi ya skuli zimejaa wanafunzi kupita kiasi, hivyo kupunguza ubora wa mazingira ya kujifunza.

Tatizo jingine ni upungufu wa bajeti fedha za elimu bado ni ndogo mno, ikilinganishwa na mahitaji ya sekta hiyo muhimu. Hali hii inakwamisha uwekezaji wa muda mrefu katika vifaa, miundombinu na miradi ya kielimu.

Mtazamo wa jamii kwa elimu ni jambo jingine na kwamba katika baadhi ya jamii, elimu haijapewa uzito unaostahili, hususan kwa watoto wa kike. Hali hii inazuia ushiriki sawa wa wanafunzi wote.

Kutokuwapo kwa mikakati ya kujifunza kutoka mafanikio ya wengine: Ni kwa sababu Zanzibar haijachukua hatua za makusudi za kujifunza kutoka mifano ya kimataifa kama Singapore na Finland, ambako elimu imekuwa nguzo kuu ya maendeleo ya kijamii na kiuchumi.

### KUIGA SINGAPORE

Singapore, ni kisiwa kilichoko Kusini Mashariki mwa Asia ambayo ni jirani na mataifa ya Thailand na Indonesia. Inasifika kielimu na inaweza kutoa somo muhimu kwa nchi kama Zanzibar.

Pamoja na kukosa rasilimali nyingi za asili, nchi hii imefanikiwa kwa sababu ya kuwekeza katika rasilimali watu kupitia mfumo bora wa elimu.

Mafanikio ya Singapore yanatokana na ubora wa walimu. Serikali inawekeza kwa kina katika mafunzo ya walimu na kuwalipa mishahara minono, hatua inayoongeza ari ya kazi.

Jambo jingine ni matumizi ya teknolojia, kila mwanafunzi Singapore ana fursa ya kutumia teknolojia ya kisasa kumsaidia kujifunza.

Mfumo bora wa upimaji wa matokeo ni jambo jingine linaloipa Singapore mafanikio inatilia mkazo ujuzi wa vitendo na ubunifu badala ya nadharia pekee.

### CHA KUFANYA

Mapendekezo ya hatua za kutatua tatizo la Zanzibar, ili kuinua kiwango cha elimu inatakiwa kwa haraka iongeze bajeti ya elimu.

Serikali inapaswa kuongeza bajeti ya elimu kwa kiwango kinachoruhusu uboreshaji wa miundombinu, vifaa, na kuimarisha maslahi ya walimu.

Aidha, kuwekeza katika mafunzo ya walimu ni lazima, ianze na programu za mafunzo endelevu zinazopaswa kuanzishwa ili kuhakikisha walimu wanaendana na mabadiliko ya kielimu na teknolojia.


Jingine ni kuboresha miundombinu kwa kujenga madarasa mapya, kuanzisha maabara bora, na kuhakikisha skuli zina vifaa vya kisasa vya kufundishia na kujifunzia.

Kutumia teknolojia ni jambo muhimu kwa Zanzibar ambayo inapaswa kuanzisha programu za elimu za kidijitali, ikiwemo mafunzo ya mtandaoni na matumizi ya vifaa vya kisasa.

Suala jingine muhimu ni kujifunza kutoka mataifa mengine. Kuweka sera za elimu zinazojifunza kutoka kwa nchi zilizofanikiwa kama Singapore na Finland.

Ni muhimu kuhamasisha ushiriki wa jamii, ni pamoja na kampeni za kuwashirikisha wazazi na jamii ili kuimarisha mtazamo wa jamii kuhusu umuhimu wa elimu bora kwa watoto wote, bila ubaguzi wa kijinsia.

Kufanya tathmini ya kina ni hatua muhimu Zanzibar inapaswa kuunda chombo huru cha kufanya tathmini ya mfumo wa elimu na kuunda mpango wa mageuzi wa muda mrefu.




Kuwekeza kwenye elimu ya nguvu kazi ili kuipa maarifa ndiko kunakoleta maendeleo.

### KUSAHAU VIPAJI

Mfumo wa elimu, kutotambua vipaji mapema ni tatizo na suluhisho lake ni muhimu. Ni ukweli kwamba mfumo wa elimu wa sasa umekuwa ukijikita zaidi katika kupima uwezo wa kukariri maarifa kwa njia ya mitihani ya darasani, huku ukipuuza vipaji na uwezo wa kipekee wa kila mwanafunzi.

Hali hii imesababisha kuwepo kizazi kikubwa cha vijana wanaofeli skuli, ilhali ukweli ni kwamba wengi wao wana vipaji adimu na adhimu ambavyo vingeibuliwa vingechangia kwa kiwango kikubwa maendeleo yao binafsi na ya jamii kama vingeendelezwa mapema.

Mfumo wa elimu wa sasa hauwezi kufanikisha maendeleo ya wanafunzi wote kwa sababu haujawekwa kutambua wala kukuza vipaji vya asili. Katika kundi la wanafunzi wanaoitwa waliofeli, kumbukeni wapo wanasoka mahiri wanaoweza kushindana kimataifa.

> Kwa mfano, wanasoka kama Lionel Messi kutoka Argentina walianza kufundwa vipaji vyao mapema kupitia mifumo bora ya kuwatambua.

Aidha, wapo mafundi stadi wa magari, waashi, na seremala wenye ustadi wa kipekee.

Ndiko wanapopatikana wanamuziki, wachoraji, na wabunifu wa mavazi ambao wangeweza kufanikisha kazi za sanaa zenye mafanikio makubwa.

Kadhalika kuna wavuvi, mabaharia na wakulima ambao wangekuwa mifano ya kuigwa katika ujasiriamali wa uzalishaji mali.

Imefeli wapi? Ni swali ambalo Zanzibar inatakiwa kujiuliza. Je, tatizo liko kwao au kwa mfumo ambao umeshindwa kuwatambua na kuwaendeleza? Jibu liko wazi ni mfumo wetu wa elimu hauwatambui na kwa kufanya hivyo, tunawapotezea muda na kuwakatisha tamaa mapema.

### VIPAJI MAPEMA

Umuhimu wa kutambua vipaji mapema unafanikisha haya, kuwajengea maisha bora, watoto. Mwanafunzi ambaye kipaji chake kinatambuliwa mapema hukuzwa katika eneo analolipenda na kulimudu, kutamwezesha kufanikisha maisha yenye tija na furaha.

Jambo jingine ni kuchangia maendeleo ya jamii, vipaji vilivyotambuliwa na kuendelezwa huweza kuchangia uchumi na maendeleo ya kijamii.

Kwa mfano, wanasoka kama Lionel Messi kutoka Argentina walianza kufundwa vipaji vyao mapema kupitia mifumo bora ya kuwatambua.

Kupunguza ukosefu wa ajira. Ikumbukwe elimu inayotambua vipaji hutengeneza wataalamu katika kila sekta, badala ya vijana wengi kusoma kwa lengo la ajira zisizoendana na uwezo wao.

Jambo jingine ni kutoa nafasi ya ubunifu: Mfumo wa kutambua vipaji hujenga jamii yenye watu wabunifu, mathalani, kama Finland, ambapo elimu haina mtihani wa mwisho wa kufeli au kufaulu, huwatambua wanafunzi kulingana na uwezo wao wa kipekee na kuwapa mwelekeo bora.

### MATAIFA YALIYOFANIKIWA

Finland ina mfumo wa elimu unaolenga kugundua uwezo wa kipekee wa kila mwanafunzi, huku ikijikita katika mafunzo ya vitendo na ubunifu. Hakuna msisitizo wa kupimwa kwa mitihani ya darasani pekee.

Singapore nayo imefanikiwa. Wanafunzi hutambuliwa mapema na kuelekezwa katika maeneo wanayoyopenda. Kwa mfano,

INAENDELEA UK.14

INATOKA UK.13

# Lazima kuchukua hatua haraka kuimarisha elimu

wanafunzi wenye uwezo wa kiufundi hupewa nafasi za kujifunza fani hizo kupitia maabara za kisasa na programu za mafunzo kwa vitendo.

Ujerumani mfumo wa "dual education" wa Ujerumani unaunganisha masomo ya darasani na mafunzo ya vitendo. Wanafunzi wenye vipaji vya kiufundi hupewa mafunzo maalum ya kazi kama uhandisi, useremala, au ufundi magari na wanapoingia kwenye soko la ajira wanakuwa na ujuzi wa moja kwa moja.

**MAPENDEKEZO KWA Z'BAR**

Kuanzisha mfumo wa kutambua vipaji mapema. Kila shule au skuli iwe na mfumo wa tathmini unaotambua vipaji vya kipekee vya wanafunzi tangu wakiwa wadogo.

Aidha, walimu wapewe mafunzo maalum ya jinsi ya kutambua uwezo wa kipekee wa wanafunzi, iwe ni sanaa, michezo, ufundi, au sayansi.

Jambo jingine ni kuboresha elimu ya ufundi na vitendo,kwa kujenga skuli za ufundi na vyuo vya mafunzo vinavyokidhi mahitaji ya vipaji tofauti kama michezo, sanaa na ufundi.

Pia, kuanzisha mashindano ya kitaifa ya vipaji kwa wanafunzi ili kuwahamasisha na kuwatambua mapema.

Kuanzisha programu za ushirikiano, ili ushirikiana na sekta binafsi na za umma kuwapa wanafunzi nafasi za mafunzo kwa vitendo (internship) katika maeneo yanayohusiana na vipaji vyao.

Jingine ni kutoa fursa kwa wanafunzi kufuata fani wanazopenda. Hapa mfumo wa elimu utoe uhuru kwa wanafunzi kuchagua fani kulingana na vipaji na shauku zao badala ya kulazimishwa kufuata masomo yanayokaririwa.

Ni muhimu kuhakikisha kuwa ushauri nasaha unapatikana kwa wanafunzi wote ili kuwapa mwongozo bora wa maisha na kazi.

Kuhamasisha familia na jamii kuheshimu vipaji ni jambo muhimu: Aidha, programu za elimu kwa wazazi na walezi kuhusu umuhimu wa kuwatambua na kuwaendeleza watoto wao kulingana na vipaji vyao.

Mafanikio ya elimu Singapore, Finland, Ujerumani na Korea Kusini: Mifano, vielelezo na mapendekezo kwa Zanzibar



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akifungua Skuli ya Sekondari Makoba, Zanzibar kwenye maadhimisho ya miaka 61 ya Mapinduzi. **PICHA: OWM**

Singapore, elimu ya kukuza ubora wa wanafunzi na ushindani wa kimataifa. Imeweka mfumo wa elimu unaojikita kwenye ubora wa masomo ya sayansi, teknolojia, uhandisi, na hisabati (STEM).

Kuna mchakato wa mapema wa kugundua uwezo wa kila mwanafunzi na kuwagawa katika ngazi tofauti za masomo kulingana na uwezo wao.

Aidha, mMfumo wa "Teach Less, Learn More" fundisha kidogo, jifunze zaidi' umeimarishwa ili walimu waweze kufundisha kwa undani na kutumia muda mrefu kushughulikia uelewa wa kina wa wanafunzi badala ya kufundisha vitu vingi kwa haraka.

**MAFANIKIO:**

Inashika nafasi ya juu duniani katika mitihani ya (Programme for International Student Assessment (PISA) na mpango wa tathmini ya mwanafunzi wa kimataifa. Mfumo wa elimu umewakuza wataalamu wa teknolojia na uhandisi, na kuchangia moja kwa moja ukuaji wa uchumi wa nchi hiyo.

**Mfano:** Mfumo wa kitaaluma wa Singapore hutoa wanafunzi wenye maarifa ya kimataifa kama vile binti wa Singapore, Lim Ding Wen (9), ambaye akiwa na miaka tisa alitengeneza programu ya teknolojia inayotumika duniani kote.

**2. Finland:** Elimu isiyo na mashindano na inayojali usawa.

Mfumo wake hauna mitihani ya kitaifa kwa wanafunzi wadogo; badala yake, hupimwa kwa miradi na mawasilisho ya ubunifu.

Walimu wanachaguliwa kwa umakini na kufundishwa katika ngazi ya juu wana elimu ya shahada ya uzamili.

Masomo ni bure, na kila mwanafunzi ana haki sawa ya elimu bora.

**Mafanikio:** Finland ni miongoni mwa nchi zinazoongoza kwa usawa wa elimu duniani. Hakuna pengo kubwa kati ya wanafunzi wa hali ya juu na wa kawaida.

Mfumo huu unatoa wanafunzi wabunifu, wenye furaha, na wenye uwezo mkubwa wa kuhimili changamoto za dunia ya kisasa.

> Mafanikio ya elimu Singapore, Finland, Ujerumani na Korea Kusini: Mifano, vielelezo na mapendekezo kwa Zanzibar

Mfano: Mfumo wa Finland unahamasisha ubunifu, na hii imeonekana kwa miradi mbalimbali ya wanafunzi wao, kama vile matumizi ya roboti kwa kazi za kijamii.

**UJERUMANI:** Mfumo wa ufundi na elimu ya kujifunza kwa vitendo.Mfumo wa "dual education" elimu pacha unaojumuisha elimu ya darasani na mafunzo ya vitendo kazini.

Wanafunzi wana uwezo wa kuchagua kati ya masomo ya kitaaluma na ya ufundi tangu wakiwa vijana wadogo.

Serikali inashirikiana na sekta binafsi kutoa nafasi za mafunzo kwa wanafunzi katika sekta kama uhandisi, teknolojia, na biashara.

**MAFANIKIO:** Ujerumani ina kiwango cha chini cha ukosefu wa ajira kwa vijana kwa sababu mfumo wa ufundi unawaandaa moja kwa moja kwa kazi.

Taifa hili limefanikiwa kuandaa na kutoa mafundi stadi na wataalamu wa sekta mbalimbali, na uchumi wa viwanda umeimarika kutokana na mchango wa mfumo wa elimu.

Mfano: Mfumo wa ufundi wa Ujerumani umewasaidia vijana kuingia kwenye soko la ajira moja kwa moja, kama vile kuwa mafundi magari kwa kampuni kubwa kama Mercedes-Benz.

**4. KOREA KUSINI:** Mfumo mkali wa nidhamu, mfumo, unaojulikana kwa mfumo wake wa nidhamu. Kuna msaada mkubwa kutoka kwa wazazi, jamii, na serikali kuhakikisha watoto wanapata elimu bora. Serikali inawekeza sana katika teknolojia ya elimu na miundombinu ya kisasa.

**MAFANIKIO:**

Wanafunzi wa Korea Kusini hushika nafasi za juu duniani katika masomo ya hisabati na sayansi. Taifa hilo limefanikiwa kuwa miongoni mwa viongozi wa dunia katika teknolojia, viwanda, na ubunifu, likichangiwa na elimu yao bora na nidhamu ya hali ya juu.

Mfano: Kampuni kama Samsung na LG zimefanikiwa kwa sababu ya mfumo wa elimu unaotoa na kuandaa wataalamu wa teknolojia na uhandisi.

***ITAENDELEA***

***Maoni +14374316747***
***Khaleed_ihaab@yahoo.com***

# Ni msako nyumba kwa nyumba kufikisha wenye ulemavu darasani

INATOKA UK.11

"Sisi tunashughulika na watoto wenye ulemavu karibu wa aina zote na wale ambao wanahitaji miwani, viti mwendo na mahitaji mengine, huwa tunawatafutia kutoka kwa wafadhili wa ndani," anasema.

Zunufa Nyasi ni mzazi wa mtoto mwenye ulemavu mwenye miaka tisa ambaye ni miongoni mwa waliohamasishwa kupeleka shule mtoto wake ambaye sasa anasoma Shule ya Msingi Rufu iliyoko Mbande Temeke.

Anasema alikata tamaa kumpeleka mtoto shule kutokana na ulemavu wake, lakini shirika hilo lilipomhamasisha ndipo akaamua kumpeleka na sasa anaendelea na shule ingawa kuna changamoto.

"Mtoto wangu hawezi kuongea wala kutembea, amepewa kiti mwendo, niliambiwa kuwa ingawa hawezi kuongea, akiwa shuleni kuna kitu anaweza kukipata, hivyo kila ninayempeleka shule anakuwa chini ya uangalizi wa walimu kwenye mazingira ya shule," anasema Zunufa.

Zunufa anasema kuwapo kwa mfumo wa elimu jumuishi kunasaidia mtoto wake kuwa katika mazingira ya shule huku yeye mzazi akiendeela na shughuli nyingine za kujitafutia riziki.

Shirika la Maendeleo ya Watoto la Umoja wa Mataifa (UNICEF) linatekeleza kuwa idadi ya watoto wanaoishi na ulemavu duniani ni milioni 240.

Vilevile, ripoti hiyo ya UNICEF ya mwaka 2021 inaeleza kuwa watoto hao wanakosa fursa ikilinganishwa na wenzao wasio na ulemavu katika hatua nyingi za ustawi wa jamii.

Pia mtoto mmoja kati ya 10 anakosa mahitaji ya msingi ikiwamo elimu, ulinzi, chakula na tiba, kwa mujibu wa UNICEF.





## Mkakati kudhibiti utupaji taka ovyo mitaani waiva

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

OFISI ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), imeandaa Mkakati wa Usimamizi wa Taka wa Mwaka 2025-2030 unaolenga kuimarisha miundombinu ya usimamizi wa taka katika maeneo yote nchini.

Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais, Abdallah Mitawi, alisema hayo juzi jijini hapa wakati akifungua kikao cha wadau kuhusu kubadilishana uzoefu wa udhibiti wa taka za plastiki nchini.

Alisema kiwango kikubwa cha taka zinazozalishwa hutupwa ovyo isipokuwa katika halmashauri saba zenye madampo ya kisasa ambazo ni Arusha, Tanga, Mwanza, Mbeya, Dodoma, Kigoma na Mtwara.

Aidha, alisema katika maeneo makubwa ya mijini, ardhi inayofaa kwa ajili ya kutupa taka inazidi kuwa adimu na ghali.

"Inakadiriwa kuwa takribani hekta 200 za ardhi zitahitajika kila mwaka ili kuhifadhi tani milioni 26 za taka kufikia mwaka 2030," alisema na kuongeza:

"Hii inaonesha umuhimu wa kuzingatia dhana ya 3Rs kwa kuanzisha vituo rejeshi vya taka ambavyo vitasaidia kutengenesha taka, kuhifadhi na kurejeleza ili zile zinazozalishwa zisiathiri mazingira bali ziongeze tija katika uchumi wa nchi yetu," alisisitiza.

Kadhalika, aliziagiza mamlaka za mikoa na serikali za mitaa kushirikiana na sekta binafsi kuandaa na kutekeleza mikakati madhubuti ya urejelezaji wa taka ikiwamo kuanzisha vituo rejeshi vya taka na kutumia fursa ya uwekezaji wa viwanda vya kuchakata taka kama chanzo cha mapato kwa halmashauri.

"Mamlaka za serikali za mitaa kuhakikisha zinatenga fedha na kutumia fedha hizo kwa ajili ya shughuli za usimamizi wa mazingira," alisema.

Vile vile, aliziagiza mamlaka za serikali za mitaa kuhakikisha zinatenga maeneo kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali za mazingira ikiwamo ujenzi wa miundombinu ya usimamizi wa taka kama vituo rejeshi (MRF) na viwanda vya kurejeleza taka.

Hata hivyo, baadhi ya wadau wa mazingira nchini, walishauri katika kiako hicho serikali kujikita katika kutafuta ufumbuzi wa taka za plastiki ambazo hazirejeshwi ili kusaidia kupunguza kuzagaa mitaani na kuwa tishio kwa mazingira.

# NEMC yabaini ongezeko la kelele Dodoma

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

BARAZA la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Kanda ya Kati limebaini ongezeko la uzalishaji wa sauti zilizozidi kiwango katika Jiji la Dodoma, zinazotokana na uendeshaji wa maeneo ya starehe, viwanda na nyumba za ibada.

Kaimu Meneja wa NEMC Kanda ya Kati, Novatus Mushi aliyasema hayo jana jijini hapa alipokuwa akizungumzia shughuli zilizofanywa na ofisi hiyo kwa kipindi cha Julai 2024 hadi Januari 2025.

Alisema kutokana na hali hiyo malalamiko kuhusu athari za sauti hizo yamekuwa yakiongezeka na kwa kuzingatia afya na usalama wa wakazi wanaoishi karibu na maeneo hayo NEMC limekuwa likiainisha maeneo yaliyo katika hatari ya kupata athari zitokanazo na viwango vikubwa vya sauti ili kushauri namna bora ya kuyasimamia na kuyafuatilia.

Aidha, alisema kati ya malalamiko yaliyowasilishwa, malalamiko yaliyohusu kelele chafuzi yalikuwa ni 14 sawa na asilimia 58 ya malalamiko yote ni ya kelele chafuzi yalihusu kelele zinazotokana na uendeshaji wa maeneo ya starehe, viwanda na nyumba za ibada na mengine 10 yalihusiana na uchafuzi na uharibifu wa mazingira katika maeneo mbalimbali ya mikoa ya Dodoma, Singida na Iringa.

Kuhusu ukaguzi wa miradi, alisema kwa kipindi cha Julai, 2024 hadi Januari, 2025, NEMC wametembelea na kukagua miradi 603 ya uwekezaji katika mikoa ya Dodoma, Iringa na Singida ikiwa ni asilimia 75 ya makadirio kwa mwaka 2024/25.

Alisema kwa kipindi hiko NEMC imegundua na kufanya tathmini shirikishi za kufuatilia uzingatiaji wa sheria ya mazingira katika miradi ya kimkakati ikiwamo Reli ya Kisasa (SGR), Mji wa Serikali - Mtumba, Barabara ya Mzunguko - Dodoma, miradi ya kilimo ya BBT, ujenzi wa Bwawa la Maji-Farkwa na Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Msalato.

Kuhusu Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM), alisema kwa kipindi hicho Ofisi ya Kanda ya Kati imesajili miradi ya maendeleo 105 na kati ya hiyo 51 imefanyiwa mapitio na kuwasilishwa kwa ajili ya kupewa vyeti vya mazingira.

Aidha, alisema vyeti 30 vilitolewa sawa na asilimia 59 ya miradi iliyowasilishwa na kufanyiwa tathmini kwa ajili ya kupewa vyeti vya mazingira.



Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano na Masoko wa Chuo cha Mipango na Maendeleo Vijijini Dodoma, Godrick Ngolly, akimwagilia mti, baada ya kuupanda kwenye eneo la Shule ya Msingi ya Buigiri Wasioona ya Chamwino jana, ikiwa sehemu ya maadhimisho ya miaka 45 tangu kuanzishwa kwa chuo hicho. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# PPAA yataka wadau ununuzi kushiriki mafunzo ya moduli

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MAMLAKA ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA) imewataka wadau wa ununuzi wa umma mikoa ya Kanda ya Ziwa kushiriki mafunzo ya matumizi ya moduli ya kuwasilisha na kushughulikia rufani na malalamiko kwa njia ya kielektroniki katika Mfumo wa Ununuzi wa Umma (NeST).

Mafunzo hayo yenye lengo la kuwanoa wanunuzi wa umma kuhusu kuufahamu mfumo huo, ili waweze kuutumia kwa ajili ya kuwasilisha malalamiko yao yamepangwa kufanyika Februari 4 hadi 6, jijini Mwanza.

Rai hiyo imetolewa jana na Katibu Mtendaji wa PPAA, James Sando wakati akizungumza na waandishi wa habari katika maonesho ya Wiki ya Sheria yanayoendelea katika viwanja vya Nyerere Square vilivyopo jijini Dodoma.

Sando, alisema mafunzo hayo yatakayoambatana na tamko rasmi la kuanza kwa matumizi ya moduli hiyo, lengo lake ni kutaka wadau wa ununuzi kuelewa mfumo huo ikiwamo kuutumia.

Alisema kuwa, Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA) kwa kushirikiana na Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA) imekamilisha moduli ya kuwasilisha na kushughulikia rufani na malalamiko kwa njia ya kielektroniki katika nfumo wa NeST.

"Mafunzo ya matumizi ya moduli kwa Kanda ya Ziwa yanawalenga wazabuni na watendaji wa taasisi nunuzi wa mikoa ya Mwanza, Shinyanga, Kagera, Musoma, Geita na Simiyu. Mafunzo yatafanyika Februari 04 hadi 06 mwaka huu jijini Mwanza," alisema Sando.

Pamoja na mambo mengine Katibu Mtendaji Sando aliongeza kuwa mafunzo hayo kuhusu matumizi ya moduli ya kuwasilisha na kushughulikia rufani na malalamiko kwa njia ya kielektroniki katika mfumo NeST yataendelea kwa kanda nyingine za Kaskazini, Kati, Nyanda za Juu Kusini pamoja Kusini.

Aidha, Sando alitoa wito kwa wadau wa kanda nyingine ambazo hazijapatiwa mafunzo kujiandaa kwani watafikiwa na kupatiwa mafunzo kuhusu matumizi ya moduli hivi karibuni katika kanda husika.

Akizungumzia kuhusiana na mfumo huo alisema, awali malalamiko na rufani zilikuwa zinawasilishwa na mzabuni kufika katika ofisi za PPAA jijini Dodoma.

Aidha, kutokana na mabadiliko ya Sheria ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2023 kuweka sharti la lazima la kufanya ununuzi wa umma kieletroniki, PPAA kwa kushirikiana na PPRA imejenga moduli itakayotumika kuwasilisha malalamiko na rufani kieletroniki bila kuwa na ulazima wa kufika katika ofisi za PPAA.

Hata hivyo alisema kabla ya mfumo huo kuanza walikuwa wakiskiliza malalamiko Kwa siku 45,lakini hivi sasa siku hizo zimepungua hadi kufikia 40 jambo ambalo ni hatua nzuri.

Mei 28 - 29, 2024 mafunzo ya matumizi ya moduli ya uwasilishaji wa malalamiko/rufaa kwa njia ya kieletroniki yaliandaliwa na PPAA kwa mikoa ya Dar es Salaam, Tanga Morogoro na Pwani.





# Tume: Ukusanyaji mapato mkoani Mbeya bado tatizo

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MKOA wa Mbeya umetajwa kuwa miongoni mwa mikoa yenye kiwango kidogo cha ukusanyaji wa kodi licha ya kuwa na idadi kubwa ya wananchi pamoja na shughuli nyingi za uzalishaji mali.

Mwenyekiti wa Tume ya Rais ya Maboresho ya Kodi, Balozi Ombeni Sefue, aliyasema hayo jana jijini Mbeya kwenye kikao cha wadau wa kodi kilichokuwa na lengo la kukusanya maoni ya kuboresha mifumo ya kodi.

Alisema Mkoa wa Mbeya una shughuli mbalimbali za uzalishaji mali ikiwamo kilimo, uchimbaji madini, ufugaji, usafirishaji, biashara na shughuli zingine, lakini kiwango cha ukusanyaji wa mapato kiko chini hali ambayo inaashiria kuwapo kwa ukwepaji wa kodi.

Alisema mkoa huo unashika nafasi ya 12 kitaifa ukipitwa na mikoa mingine ambayo haina vyanzo vingi vya mapato na hivyo akawataka wadau kubadilika na kuanza kulipa kodi kwa maelezo kuwa kodi hizo ni kwa ajili ya maendeleo ya taifa.

"Lakini pamoja na hali hii Mkoa wa Mbeya ni miongoni mwa mikoa ambayo inachangia kwa kiasi kikubwa ukuaji wa pato la taifa, mkoa huu unashika nafasi ya tatu na unachangia Sh. trilioni 10.75 kiwango ambacho ni kikubwa," alisema Balozi Sefue.

Aliwataka wadau wa kodi kuwasilisha maoni ya namna ya kuboresha kodi kwa njia mbalimbali ikiwamo barua pepe, kupiga simu na ama kuwasilisha maoni kwa njia ya maandishi.

Baadhi ya wadau waliomba serikali kupunguza utitiri wa kodi kwenye biashara ili biashara ziendelee kustawi na ukusanyaji wa mapato uongezeke.

Mwenyekiti wa Chemba ya Wafanyabiashara, wenye Viwanda na Wakulima (TCCIA), Erick Sichinga alisema kuna baadhi ya taasisi za serikali na mamlaka ambazo kwa mujibu wa sheria zilitakiwa kutoa huduma kwa wananchi lakini zimegeuka zikitoza kodi.

Alisema baadhi ya taasisi hizo ni Jeshi la Zimamoto na Uokoaji ambalo limekuwa likiwatoza wafanyabiashara mapato yanayohusu huduma ya zimamoto kila mwaka pamoja na kuwauzia wafanyabiashara baadhi ya vifaa vya kuzimia moto.

Vilevile alisema jeshi hilo limekuwa likiwatisha wafanyabiashara wakati wa kukagua vifaa hivyo na kuwatoza faini inapotokea taasisi zao hazina vifaa vya kuzimia moto.

Mwenyekiti wa Jumuiya ya Chama cha Wachimbaji Mkoa wa Mbeya (MBEREMA), Leonard Manyesha, alisema kwenye sekta ya madini wamekuwa wakitozwa kodi nyingi ambazo baadhi zimegeuka kuwa kero kwa wachimbaji.

Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wafanyabiashara Mkoa wa Mbeya, Pascal Mahuve, alisema baadhi ya wafanyabiashara wamekuwa wakifunga biashara zao kutokana na utitiri wa kodi kutoka kwa taasisi za serikali.



Mwenyekiti wa Tume ya Rais ya Maboresho ya Kodi, Balozi Ombeni Sefue akizungumza na wadau wa kodi wa Mkoa wa Mbeya jana, wakati wa kikao cha kukusanya maoni ya namna ya kuboresha kodi. Kulia ni Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Beno Malisa na (kushoto) ni Mjumbe wa Tume hiyo, David Tarimo. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## Wapatiwa elimu kutokomeza udumavu kwa watoto

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WANANCHI wa Kijiji cha Inyala kilichoko Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, wameanza kupatiwa elimu ya kukabiliana na tatizo la udumavu kwa watoto kwa lengo la kupunguza tatizo hilo.

Elimu hiyo inatolewa na shirika lisilokuwa la kiserikali la ADP Mbozi ambapo wananchi hao wanapatiwa elimu kuhusu uandaaji wa chakula kwa ajili ya watoto.

Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii wa shirika hilo, Maneno Uledi alisema elimu hiyo inalenga kuwasaidia wakulima kujua namna ya kuandaa lishe kwa watoto, ili kupunguza kiwango cha udumavu ndani ya wilaya hiyo.

Alisema elimu hiyo mbali na kutolewa kwa wananchi pia wanaitoa kwenye maeneo mengine ikiwamo kwenye taasisi za elimu ili kuhakikisha elimu hiyo inasambaa kwa kasi zaidi.

"Tunashirikiana kwa kiwango kikubwa na serikali kutoa elimu hiii na lengo ni kupunguza tatizo hili la udumavu pamoja na kupunguza matatizo yanayotokana na udumavu kwa watoto," alisema Uledi.

Ofisa Lishe wa Wilaya ya Mbeya, Namkundaelly Mmbaga, alilishukuru shirika hilo kwa kujitolea kutoa elimu kwa wananchi hao akidai kuwa itasaidia kutimiza malengo ya serikali ya kupunguza tatizo la udumavu kwa watoto.

Alisema udumavu kwa watoto unasababisha matatizo mengine ikiwamo magonjwa kwa watoto, kupungua kwa uzalishaji pamoja na kupungua kwa kiwango cha elimu.

"Sisi kama halmashauri tuna mikakati yetu ambayo tunatekeleza ya kupunguza udumavu, lakini huu utaratibu wenu mlioanzisha utatusaidia kufikia malengo yetu," alisema Mmbaga.

Hivyo, aliwataka wananchi kuendelea kufuata taratibu zote ambazo wataalamu hao wamewaelimisha ili kuhakikisha watoto wao wanakuwa na afya njema.

# Matumaini mapya mradi wa maji ukikamilika

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAKAZI wa Kata ya Mjele katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, wameondokana na adha ya kutembea umbali mrefu kwenda kutafuta huduma ya maji baada ya serikali kukamilisha mradi wa maji wa Mshewe-Mjele.

Wakizungumza na Nipashe mwishoni mwa wiki, wananchi hao walisema kabla ya mradi huo kukamilika walikuwa wanatumia muda mrefu kwenda kutafuta maji kwenye makorongo na kwenye mito, hali ambayo ilikuwa inasababisha washindwe kutekeleza baadhi ya majiukumu.

Shupati Sinkwembe alisema walikuwa wanakwenda kuchota maji usiku kwenye makorongo ambako walikuwa wanakoswa kung'atwa na nyoka na wanyama wengine wakali wakiwamo fisi.

Alisema kwa sasa maji yanapatikana kwa wingi katika eneo hilo na kwamba baadhi ya wananchi wenye uwezo wameingiza kwenye nyumba zao na hivyo tatizo la kupoteza muda kwenda kutafuta huduma hiyo limepungua.

Alisema uwepo wa huduma hiyo umesaidia hata wananchi kuanza kujenga nyumba nzuri kwa maelezo kuwa wanayatumia maji hayo kufyatua matofali kwa ajili ya kujenga nyumba.

Alisema wakazi wa vitongoji vya pembezoni ambavyo bado havijafikiwa na huduma hiyo wanalazimika kubeba maji hayo kwa kutumia pikipiki, kichwani na kusafirisha kwa kutumia wanyamakazi hasa punda.

Upendo Emmanuel alisema walikuwa wanapata shida zaidi kipindi cha kiangazi akidai kuwa hata maji ya kwenye makorongo huwa yanakauka na hivyo kusababisha wagombanie maji ya kwenye visima ambavyo vimechimbwa kwenye chemchemi.

Alisema eneo hilo ni kame na kwamba ndiyo sababu iliyoifanya serikali kuchukua maji kutoka katika Kijiji cha Mshewe ambacho kipo umbali wa zaidi ya kilomita 20 kutoka katika kijiji chao.

Mmoja wa vijana wanaoendesha pikipiki katika kata hiyo, Nijalie Gunza alisema kutokana na uwepo wa mradi huo amepata ajira ya kupeleka maji kwa baadhi ya wananchi kila siku na hivyo kujipatia kipato cha kuendeshea maisha.

Diwani wa Kata ya Mjele, Tatizo Gunza alisema kata yake ina vijiji vitatu ambavyo vyote vimeshaunganishiwa huduma hiyo ya maji na hivyo kuwapunguzia wananchi shida ya upatikanaji wa maji.





## Waziri apendekeza uanzishaji miamala fedha za kigeni

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji, Sharif Ali Sharif, amesema umefika wakati sasa kuwa na miamala ya fedha za kigeni, ili Watanzania wanaoishi nje ya nchi kutuma fedha kwa ajili ya kusaidia katika sekta za maendeleo.

Alitoa rai hiyo juzi wakati akizindua huduma ya miamala ya fedha kwa njia ya kidigitali visiwani hapa.

Alisema kuna Watanzania wapo nje ya nchi na wanataka kutuma fedha kwa ndugu zao hapa nchini kupitia miamala ya kidijitali.

Hivyo kunapaswa kuwa na miamala ya fedha za kigeni kwa sababu Watanzania hao wanamsaada mkubwa katika nchi, jamii, familia zao na kwa ajili ya uwekezaji.

"Nishauri kwamba mfanye bidii ya kuhakikisha na wao wanaguswa na wanaweza kutumia fursa hii tuliyonayo dunia nzima," alisema Sharif.

Sharif alisema dunia inapiga vita utakatishaji wa fedha hivyo ni vyema huduma hiyo kuhakikisha jambo hilo halitatokea.

Aidha, alisema huduma hiyo ya miamala inatoa fursa kwa vijana kupata ajira na kuendana na mipango na dira ya Serikali ya Zanzibar na ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Naibu Kamishna Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) Zanzibar, Saleh Haji Pandu, alisema dunia ya sasa siyo salama kuwa na pesa mkononi kwa sababu ya uwepo wa matukio mengi ya ujambazi na majanga ya moto.

Hivyo, huduma hiyo ni nafasi nzuri ya kuitumia ili kuhakikisha fedha zinakuwa salama.

Mjumbe wa Bodi wa Azam Pesa, Khalfani Abdallah, alisema sekta ya fedha ina maendeleo makubwa katika kuchangia uchumi wa nchi na kuwawezesha wananchi kupata huduma mbalimbali za kifedha.

Alisema katika kupanuka kwa huduma za kifedha Tanzania, wananchi wengi wanaweka fedha zao katika simu (pochi la kidigital) lakini kumekuwa na ukosefu wa huduma ambazo wananchi wanaweza kutumia wakiwa na faraja na amani.

Alisema kuwa teknolojia hiyo wananchi watakuwa na uhakika wa usimamizi wa fedha zao ambao unasimamiwa kwa misingi ya sheria na uadilifu.

# Ofisi ya AG yatafuta dawa kumaliza ukatili kijinsia

**Na Mwandishi Wetu**

OFISI ya Mwanasheria Mkuu Zanzibar imesema inaendelea na kutafuta njia bora za kudhibiti ukatili wa kijinsia, ikiwa ni pamoja na kuanzisha sheria mpya ili kushughulikia changamoto za matukio hayo yanayoendelea kujitokeza nchini.

Wakili wa Serikali, Dk. Abdulnasser Hikmany alisema hayo juzi visiwani Zanzibar wakati akifungua kikao cha kukusanya maoni kuhusiana na utafiti wa masuala ya ukatili wa kijinsia.

Alisema hatua hiyo inatokana na vitendo hivyo kukosa sheria na miongozo ya moja kwa moja ya kuvidhibiti na kusababisha kushamiri kwa matukio hayo siku hadi siku.

Dk. Abdulnasser alisema baada ya kufanyika utafiti wa kuangalia mifumo ya kisheria inayohusiana na udhibiti wa masuala ya ukatili wa kijinsia na kubaini changamoto mbali mbali, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu imekuja na mapendekezo ya kisheria na kiutendaji ili kudhibiti vitendo hivyo.

Aidha, aliwataka wadau hao kutoa michango yao katika mapendekezo hayo na kuahidi kupokelewa na kufanyiwa kazi.

Akiwasilisha mapendekezo hayo, Wakili wa Serikali Mkuu, Dk. Mahfoudha Masoud Ali, alisema mapendekezo hayo yametokana na masuala yaliyoibuka kwenye utafiti uliofanywa kuangalia sheria zilizopo, uzoefu wa sheria za nchi mbalimbali, mikataba ya kimataifa, sheria za ndani, sera, miongozo na maoni ya wadau.

Alisema kuwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu imependekeza kuanzishwa kwa vituo vya waathirika wa ukatili wa kijinsia, kuwafanyia tathmini, kuwarekebisha pamoja na kuwapo wajibu wa kuwajuulisha haki zao ili kukabiliana na janga hilo.

Baadhi ya wadau wa masuala ya ukatili wa kijinsia walioshiriki kikao hicho walisema kupatikana kwa sheria mpya ya kudhibiti vitendo vya ukatili wa kijinsia kutasaidia kupunguza vitendo hivyo endapo sheria hiyo itatekelezwa ipasavyo.

Mkurugenzi wa Jumuiya ya Wajane Zanzibar (ZAWIO), Tabia Makame Mohammed, alisema uzoefu unaonesha kuwa hakuna usimamizi katika sheria zilizopo jambo linalopelekea vitendo hivyo kutokisha na kushauri kutekelezwa ipasavyo sheria, huku wakisubiria sheria yenye nguvu dhidi ya janga hilo.

Mtabibu wa Saikolojia kutoka Kitengo cha Afya ya Akili, Mohammed Sharif Haji, alisema sheria zilizopo zilijikita kuwafikisha waathirika katika vyombo vya sheria na kupata haki zao bila kuzingatia matibabu ambayo huathirika zaidi kutokana na matendo hayo.

Meneja Uendeshaji wa Umoja wa Watu wenye Ulemavu Zanzibar, Donal Godwin Naveta, aliwashauri kuliangalia suala la kupewa kipaumbele kwa waathirika kwani linaweza kuchangia kuongeza kwa kesi za kusingiziwa.




Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Exim, Jaffari Matundu (katikati), akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam hivi karibuni, wakati akitangaza Ripoti ya Fedha ya 2024 ya benki hiyo, ikionesha mafanikio makubwa ya kifedha na ukuaji endelevu. Kushoto ni Mkuu wa Kitengo cha Huduma za Rejareja, Andrew Lyimo, na Ofisa Mkuu wa Fedha, Shani Kinswaga. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Serikali yataja lengo uanzishaji mfuko huduma afya kwa wote

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Afya, Nassor Ahmmed Mazrui amesema malengo ya serikali ya kuanzisha Mfuko wa Huduma ya Afya kwa Wote ni kuwapatia wananchi huduma bora ya afya na ya uhakika.

Alisema hayo juzi Darajani Visiwani Zanzibar wakati akizindua usajili wa sekta isiyo rasmi na makundi mengine katika Mfuko wa Huduma za Afya Zanzibar.

Alisema kuwa mwaka 2023 serikali ilianzisha mfuko huo kwa lengo la kuhakikisha kuwa upatikanaji wa huduma bora za afya zinakuwa endelevu kwa wananchi wote wa Zanzibar.

Mazrui alisema tayari mfuko huo umeshakamilisha usajili wa wanachama kutoka sekta za umma na upo katika hatua za kukamilisha kwa sekta binafsi, ili kuendana na sera ya serikali ya afya bora kwa wote.

"Hakuna mtu au kikundi cha watu wasiofahamu kuwa sera ya serikali ni kutoa huduma bora kwa wote na sisi tunalitekeleza hilo kwa vitendo," alisema.

Alisema serikali inafahamu kuwa afya za wananchi wake ni muhimu, ndiyo maana wakaanzisha mfuko huo ili kila mwananchi mwenye uwezo kujiunga na waliokuwa hawana uwezo serikali kuwasaidia.

Alisema suala la kujiunga na mfuko huo lina umuhimu mkubwa na hata mataifa yaliyoendelea wamekuwa na mifuko kama hiyo, hivyo ni wajibu wa wanajamii kujiunga ili kupata afya bora katika vituo.

Alisema kuwa mfuko huo utawahusu watu wote hata wageni wanaoishi Zanzibar kwa zaidi ya miezi sita. Alisema serikali imedhamiria kujenga hospitali za mikoa kwa Unguja na Pemba na Hospitali ya Taifa ya Binguni kwa lengo la kuhakikisha wananchi wake wanapata huduma bora za afya.

Mkurugenzi Mkuu wa mfuko huo, Yassin Ameir Juma alisema kuwa malengo ya kuanzishwa kwa mfuko huo ni kuwapatia huduma bora za afya wananchi wote wa Zanzibar.

Alisema kuwa mfuko huo umetoa rukhsa kwa wanajamii kuwasajili watoto wao na wazee wao tofauti na mifuko mingine, hivyo wakati umefika kwa wanajamii kuona umuhimu wa kujiunga na mfuko huo.

Alisema kuwa licha ya mfuko huo kuonekana kwenda vizuri na kufikia malengo yake lakini bado kuna changamoto kwa baadhi ya vituo vya afya vya hospitali binafsi kufanya udanganyifu katika utoaji wa huduma zao za kiafya.

Kaimu Meneja mradi wa G12 Health Programme, Erick Masoffe, alisema kupitia Serikali ya Ujerumani na Uswiss wataendelea kuunga mkono jitihada za Serikali ya Zanzibar kupitia mfuko huo.

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**MAGRETH THADEUS KASAPILA**, Anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha Nne chenye Index namba **S0549-0063** Kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia shule ya secondari Lugoba Mwaka 2016. Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo cha Polisi. TAARIFA YA POLISI: **PHQ/DOD/DOD/3922/2025**

## KUPOTEA KWA CHETI



**OMARI HUSSEIN MKAMBARA** anatangaza kupotelewa na cheti cha darasa la saba chenye index namba **PS 0204086/019** kilichotolewa na **GRACE PRIMARY SCHOOL** mwaka 2021. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/KIN/7896/2025.**

## KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA



**CHARLES AKWILINE MAKOI,** naomba kutangaza kupotelewa na hati yangu ya kusafiria namba **TAE353312** tarehe ya kutolewa sijui imeibiwa tarehe 12/12/2024. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **PHQ/KIL/MOS/2421/2025.**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**HAMISI ALLY MZAVA**

Anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki aina ya **Fekon** yenye namba ya usajili **T 132 CJW.** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi kilichopo karibu nae.

TAARIFA YA POLISI:

**PHQ/TAN/LUS/801/2025**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**JOVITH LUGOSHOLA BYARUGABA**

Anatangaza kupotelewa kwa kadi ya pikipiki, yenye namba za usajili **MC 926 ECT.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilicho karibu nayeye.

**PHQ/MOR/MOR/3027/2025**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**CATHERINE BARAKA ARON**

Anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T.286 CSL** yenye Chassis No. **RZH1241002160** na Engine No.**1RZE1002160,** Model No. **RZH124** aina ya **TOYOTA HIACE** yenye rangi **MULTICOLOUR.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilichopo jirani yake.

Taarifa ya Polisi:

**PHQ/SHI/KAH/80/2025.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**LETSHEGO FAIDIKA BANK**

inatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 587 EBE.**

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi:

**PHQ/DAR/KIN/12786/2025.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**LETSHEGO FAIDIKA BANK** inatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 233 CVL.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi:

**PHQ/DAR/KIN/12814/2025.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**RAMADHAN SAIDI SIMBA**

anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 701 CUZ – TOYOTA IST.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

Taarifa ya polisi:

**PHQ/KIL/HAI/2311/2025.**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA YA MWANZO YA WILAYA YA TARIME**

**KITUO CHA SIRARI MKOA WA MARA**

**SHAURI LA MIRATHI NAMBA 01/2025**

**JOSEPH NYAMGINI NYABAGAKA NA**
**STELLA WILLIAM MUNISI..........................WAOMBAJI**

**DHIDI YA**

**ALFRED JOHN SAGHI.................................MAREHEMU**

**KWA: YEYOTE ANAYEHUSIKA**

**KUITWA SHAURINI**

WAOMBAJI TAJWA HAPO JUU WAMEFUNGUA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU ALFRED JOHN SAGHI KATIKA MAHAKAMA HII. HATI ZA MIRATHI ZINAPATIKANA KATIKA MAHAKAMA HII.

TUNAOMBA YEYOTE MWENYE PINGAMIZI KATIKA MIRATHI HII ANATAKIWA KUHUDHURIA MAHAKAMANI TAREHE 21/02/2025. MNATAKIWA KUHUDHURIA NYINYI BINAFSI AU WAKILI WENU KISHERIA. ZINGATIA KWAMBA KUTOKUFIKA KWENU KWA TAREHE TAJWA, KESI HII ITAENDELEA KUSIKILIZWA BILA NYINYI KUWEPO MAHAKAMANI NA KUTOLEWA MAAMUZI.

IMETOLEWA KWA MKONO WANGU NA MUHURI WA MAHAKAMA HII LEO TAREHE 21/01/2025

**HAKIMU MKAZI**
**MAHAKAMA YA MWANZO**
**SIRARI**

---

**IN THE DISTRICT DELEGETE COURT OF LONGIDO**
**AT LONGIDO**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 5873 OF 2025**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE**
**LOISHIYE EMMANUEL LUKA**

**AND**

**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY**
**YESE EMMANUEL LUKA**

**GENERAL CITATION**
**(Made under Rule 75 of the Probate Rules)**

ALL PERSON claiming to have any interest in the estate of above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named petitioner. Objections to the grant should be filed on or before the 26 day of February, 2025.

Dated at LONGIDO this 28 day of January, 2025.

PRINCIPAL RESIDENT MAGISTRATE
LONGIDO DISTRICT COURT
..............................................
RESIDENT MAGISTRATE.

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA YA WILAYA YA MWANGA**

**UTHIBITISHO NA USIMAMIZI WA MIRATHI**

**SHAURI LA MIRTHI NA. 560 YA MWAKA 2025**

**MAOMBI YA BARUA YA USIMAMIAJI WA MIRATHI YA**
**ELIUD GURISHAEL MSUYA..............MAREHEMU**

**LILIAN ELIUDY MSUYA...............MUOMBAJI**

**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(Kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki katika mirathi ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa barua ya usimamiaji wa mirathi kwa muombaji aliyeomba hapo juu.

Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikwa mnamo au kabla ya tarehe 17 Mwezi FEBRUARI Mwaka 2025.

Imewasilishwa Mwanga leo tarehe 28 Mwezi JANUARI Mwaka 2025.

DISTRICT COURT MWANGA

..............................................
HAKIMU MKAZI MKUU
MAHAKAMA YA WILAYA
MWANGA
Principal Resident Magistrate I/c
Mwanga

---

**OFISI ZA MATANGAZO**

**MIKOCHENI INDUSTRIAL AREA,**

**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**

**MOB: +255 - 745 700 710.**

**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**

**website: www.ippmedia.com**

KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTEA KWA CHETI, KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI.

TUPIGIE: +255 - 0677 020701

AU

TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO,MIKOCHENI INDUSTRIAL AREA,

PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.

E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Sababu Trump kuzuia misaada Afrika Kusini

Na Maulid Mmbaga

RAIS wa Marekani, Donald Trump, amedai kuwa kumekuwa na vitendo vya kuwadhulumu wakulima wa kizungu nchini Afrika Kusini, huku akisema atakata ufadhili wowote kwa nchi hiyo hadi hapo suala hilo litakapochunguzwa.

Kwa mujibu wa Reuters Rais Trump alichapisha jana kwenye mtandao wake wa Truth Social Post akiandika "Afrika Kusini inanyakua ardhi, na inawatendea watu wa tabaka fulani vibaya sana".

Saa chache baada ya kauli hiyo, Rais wa Afrika Kusini, Cyril Ramaphosa alimjibu akisema taifa hilo linaongozwa kwa demokrasia ya kikatiba ambayo imekita mizizi kwenye utawala wa sheria, haki na usawa. Na kwamba serikali yake haijanyakua ardhi yoyote.

Rais Ramaphosa alimtaka Trump aache kuingilia masuala ya ndani ya Afrika Kusini kwa kuwa hayamhusu. Akisisitiza kuwa ardhi ya Afrika Kusini ni ya raia wa nchi hiyo, na Trump hana mamlaka ya kuwapangia cha kufanya.

"Hii ni ardhi yetu, sijui Donald Trump anahusika vipi au atafanya nini kuhusu ardhi ya Afrika Kusini kwa sababu hajawahi kuwa hapa. Aitunze Marekani yake, nasi tutaitunza Afrika Kusini yetu. Afrika Kusini ni ardhi yetu na inamilikiwa na watu wote wanaoishi hapa, siyo ya Trump," alisema Ramaphosa.

Rais Trump alisema, "Marekani haitanyamaza wala kusimama kwa hilo, tutachukua hatua. Pia, nitakata ufadhili wote ujao kwa Afrika Kusini hadi uchunguzi kamili wa hali hii utakapokamilika".

Data ya hivi karibuni ya serikali ya Marekani ilionyesha kuwa Marekani ilitoa karibu dola milioni 440 zaidi ya Sh. Trilioni 1.1 kwa ajili ya msaada kwa Afrika Kusini mwaka 2023.

Kwa sasa Afrika Kusini inashikilia wadhifa wa urais kwa muungano wa nchi zenye nguvu duniani G20, na kwamba baada ya hapo Marekani itachukua madaraka.

Kathalika mwezi uliopita, Rais Ramaphosa alisema hana wasiwasi kuhusu uhusiano wa nchi hiyo na Trump. Akisema alizungumza na Trump baada ya ushindi wa uchaguzi mkuu na anatazamia kufanya kazi na utawala wake.



Kushoto ni Rais wa Afrika Kusini, Cyril Ramaphosa, kulia Rais wa Marekani, Donald Trump. **PICHA: MTANDAO**

"Tunatazamia kushirikiana na utawala wa Trump kuhusu sera yetu ya mageuzi ya ardhi na masuala ya maslahi ya nchi mbili," alisema Rais Ramaphosa.

Pia alisema wakati Marekani ilikuwa mshirika mkuu wa kimkakati wa kisiasa na kibiashara, haikutoa ufadhili mkubwa kwa Afrika Kusini kando na mpango mkubwa wa misaada ya Virusi vya Ukimwi (VVU) na Ukimwi.

Malalamiko ya muda mrefu ya Trump, ambayo pia alikuwa ametoa mwaka 2018 wakati wa muhula wake wa kwanza, yanarudi kwenye mageuzi tata ya ardhi nchini Afrika Kusini.

Awali, sera za kibaguzi za zamani ziliwaondoa kwa nguvu Waafrika Kusini weusi na wasio weupe kutoka kwenye ardhi kwa matumizi ya Wazungu.

Ilielezwa kuwa kumekuwa na kipengele cha ugawaji na urejeshaji ardhi katika katiba ya nchi hiyo tangu Afrika Kusini ilipoibuka kutoka enzi ya ubaguzi wa rangi na kufanya uchaguzi wake wa kwanza wa kidemokrasia mwaka 1994.

Hata hivyo, ilielezwa kuwa ukosefu wa ajira na umaskini unasalia kuwa mbaya miongoni mwa Waafrika Kusini weusi, ambao ni karibu asilimia 80 ya wakazi, lakini wanamiliki sehemu ndogo ya ardhi.

Januari mwaka huu, Rais Ramaphosa alitia saini mswada kuwa sheria ambao unaweka miongozo mipya ya umiliki wa ardhi, ikiwa ni pamoja na kuwezesha serikali kuchukua ardhi bila fidia katika baadhi ya kesi.

Katika chapisho lake la X jana, Rais Ramaphosa alisema sheria hiyo sio chombo cha kutaifisha, lakini ni mchakato wa kisheria unaohakikisha upatikanaji wa ardhi kwa umma kwa njia ya usawa na haki kama inavyoelekezwa na katiba.

Vile vile, ilielezwa kuwa ulinzi wa kikatiba dhidi ya uchukuaji wa ardhi bila fidia bado unabaki pale pale, na wataalam wanaamini kuwa chama tawala cha Afrika Kusini kitakabiliwa na changamoto za kisheria ikiwa kinataka kutekeleza sera hiyo.

### MAJADILIANO

Kwenye taarifa iliyotolewa na ofisi ya Rais Ramaphosa alisema serikali yake itafungua milango ya majadiliano na utawala wa Rais Trump kuhusiana na sera ya mageuzi ya usimamizi wa ardhi na masuala mengine ya pamoja baina ya nchi hizo mbili.

Alisema anatumai kupitia mazungumzo pande hizo mbili zitafikia mwafaka na maelewano kuhusu masuala hayo.

Trump aliituhumu Afrika Kusini kutumia sera ya usimamizi wa ardhi kutaifisha ardhi ya makundi fulani ya watu nchini humo na kusema amefikia uamuzi wa kulichukulia hilo hatua.

Mgawanyo wa ardhi ni moja ya masuala yanayodaiwa kuwa na mkanganyiko nchini Afrika Kusini huku raia wengi weusi wakilalamika kuwa makundi ya raia wachache wa kizungu wanamiliki sehemu kubwa ya ardhi ya nchi hiyo.

### MAONI YA WANANCHI

Mtumia mtandao aliyesomeka kama Contrarian Owl, alieleza mtazamo wake kuhusiana na suala hilo akisema, ikiwa serikali inataka kuchukua ardhi, njia sahihi ni kulipa thamani ya soko la haki kwa mwenye mali. Na kwamba hivyo ndivyo inafanywa ulimwenguni kote.

"Umeanzisha mfumo wa ukandamizaji wa ngazi mbili katika jimbo lako. Sera zako zitafukarisha taifa lako na unajua hilo. Haihitaji kufikiri kwa kiwango cha juu kutambua kuwa unafuata hatua za kuharibu usambazaji wa chakula katika taifa lako. Unaigeuza Afrika Kusini kuwa Rwanda.

"Serikali ya Marekani inapaswa kukata mara moja misaada yote, kila senti, na kuweka vikwazo vikali kwa Afrika Kusini kwa chuki yake ya rangi na kukataa kuheshimu haki za kumiliki mali kwa misingi ya rangi," aliandika Owl.

Naye, Mulungisi Dube alisema wana dhuluma za kihistoria ambako mababu wa binamu wao kutoka Ulaya walikuja Afrika, Amerika ya Kusini na Kaskazini, Australia na sehemu nyingine za dunia na kunyakua ardhi iliyokuwa inashikiliwa na wakazi wa eneo husika.

"Sasa tunakubali kuwa sisi ni watu wamoja, tugawane, sio lazima tuwafukuze waliorithi ardhi ya wizi. Ardhi inaweza kuwa na tija tu ikiwa inashikiliwa na wale walioichukua miaka 300 au 400 iliyopita? Ikirudishwa kwa vizazi vilivyokuwepo hapo miaka elfu moja kabla, je, ni dhulma?" alihoji.

"Trump ni mkorofi tu na mbaguzi wa rangi sawa na yule anayeshikilia ardhi, ni wakati wa chochote ambacho wenyeji watafanya na ardhi ni hadithi ya siku nyingine kwa sasa waache ni yao kwa kuanzia," alisema. **Chanzo mtandao**

## INEC yaonya wanasiasa uandikishaji wapigakura

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

TUME Huru ya Uchaguzi (INEC) imewataka viongozi wa vyama vya siasa kutoingilia utekelezaji majukumu ya watendaji wa vituo wakati wa uandikishaji wapigakura.

Mjini Kibaha juzi, Kaimu Mkurugenzi wa INEC, Mtibora Selemani, alitoa onyo hilo alipozungumza kwenye mkutano wa tume hiyo na wadau wa uchaguzi kuhusu uboreshaji Daftari la Kudumu la Wapigakura.

Selemani alisema tume inategemea kuona viongozi wa vyama vya siasa wakiwahamasisha wanachama, wafuasi na mashabiki kujitokeza kwa siku saba zilizopangwa kuhakiki taarifa zao badala ya kuanza kulalamikia kuongezwa kwa siku zaidi.

Kaimu Mkurugenzi huyo alibainisha kwamba wapigakura 594,494 wanatarajiwa kuondolewa kwenye daftari kwa kukosa sifa za kuendelea kuwa kwenye daftari hilo.

Pia alieleza kwamba baada ya uboreshaji wa daftari, kutakuwa na wapigakura 34,746,638 kwa kuzingatia matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022 ambapo wapigakura wapya 5,586,433 wanatarajiwa kuandikishwa sawa na asilimia 18.7 ya wapigakura 29,754,433 waliokuwa kwenye daftari baada ya uboreshaji mwaka 2019/20.

Pia alisema wapigakura 4,369,531 wanatarajiwa kuboresha taarifa zao katika maeneo mbalimbali nchini. Tume hiyo imeridhia mabadiliko ya idadi ya vituo vya kuandikisha wapigakura kutoka 40,126 hadi 40,170 kwa kurejeaha vituo 44 vya kata 11 za Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro.

Tume hiyo ambayo imewakutanisha wadau mbalimbali wa uchaguzi mkoani Pwani kushiriki uboreshaji Daftari la Kudumu la Wapigakura katika utekelezaji unaotarajia kuanza Februari 13 hadi 19 mwaka huu.

Awali akifungua mkutano huo, Makamu Mwenyekiti wa Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi, Jaji Mstaafu Mbarouk Mbarouk, alisema lengo la mkutano huo ni kuanza maandalizi ya uboreshaji daftari hilo mkoani Pwani. Mbarouk alisema kuwa kwa sasa tume imeanza maandalizi ya mzunguko wa 11 kati ya mizunguko 13 ya uboreshaji daftari ambapo mzunguko wa 11 unahusisha mikoa ya Pwani na Tanga.

Mbarouk alisema zoezi hilo lilianza na mikoa mitatu ya Kigoma, Tabora na Katavi, lakini mpaka sasa tayari tume imeshakamilisha uboreshaji huo katika mikoa 25, ikiwamo mitano ya Zanzibar.

HABARI MICHEZO

# ZIMAMOTO YAIPUNGUZA KASI MLANDEGE FC LIGI KUU Z'BAR

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

SARE zimetawala katika michezo miwili ya Ligi Kuu Zanzibar iliyochezwa juzi Jumapili katika Uwanja wa Cairo, Kiwengwa Kisiwani hapa.

**Majira ya saa nane mchana vinara wa Ligi Kuu Zanzibar, Mlandege FC, walilazimisha sare ya bao 1-1 dhidi ya Maafande wa Zimamoto SC.**

Katika mchezo mwingine uliopigwa majira ya saa 10 alasiri majirani wawili Mwembe Makumbi City na JKU SC nao walipimana nguvu kwa kutoka sare ya bao 1-1.

Akizungumza na gazeti hili, Kocha Mkuu wa vinara wa ligi hiyo, Mlandege FC, Hassan Ramadhan, alisema hayakuwa matokeo waliyoyatarajia, lakini hawayabezi kutokana na ugumu wa mchezo ulivyokuwa uwanjani.

Alisema mchezo huo ulikuwa mgumu kwa dakika zote 90 na timu zote zilikuwa imara hadi mwisho wa mchezo huo.

Alisema wachezaji wake walicheza vizuri na licha ya kutanguliwa kufungwa, waliendelea kujituma mpaka walipofanikisha kusawazisha.

"Mchezo ulikuwa mgumu na upinzani mkali sana, katika mzunguko wa kwanza walitufunga, hivyo leo wapinzani wetu walikuja wakiwa na ari ya kuhakikisha wanatufunga pia,"alisema.

Alisema kumalizika kwa mchezo huo ni kuanza kujiandaa kwa mechi ya mzunguko unaofuata ambao watakuwa ugenini Kisiwani Pemba dhidi ya Chipukizi FC.

Kwingineko katika Uwanja wa Finya, Kisiwani Pemba, timu ya Junguni United ilifanikiwa kujinasua katika mstari wa hatari wa kushuka daraja baada ya kutoka na ushindi wa bao 3-2 dhidi ya Chipukizi FC.

Ligi Kuu Zanzibar mzunguko wa 17 utaendelea keshokutwa, Alhamisi kwa kupigwa michezo miwili ambapo waburuza mkia, Inter Zanzibar FC, watawavaa JKU SC, wakati Pemba Junguni FC watawaalika Uhamiaji FC.

## MAGIFT YA KUGIFT...



Mkulima kutoka Manyara, Ibrahim Njeja, akiwa na mkewe ndani ya gari aina ya Kia Seltos aliloshinda katika Kampeni ya 'Magift ya Kugift', inayoendeshwa na Kampuni ya Mawasiliano ya Yas Tanzania. Gari hilo alikabidhiwa mwishoni mwa wiki akiwa Msitu wa Tembo, Manyara. **NA MPIGAPICHA WETU**

# *Kipa Kagera Sugar ataja kinachowatafuna*

**Na Adam Fungamwango**

GOLIKIPA wa Kagera Sugar, Ramadhani Chalamanda, amesema timu yao imekuwa ikifanya vibaya kwenye mechi za Ligi Kuu kutokana na makosa binafsi ya wachezaji na si kitu kingine.

Kipa huyo namba moja wa timu hiyo, aliyasema hayo siku moja tu baada ya mchezo wa Ligi Kuu kati ya timu yake na Yanga, uliochezwa Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam, ambapo alikaa langoni na kulambishwa mabao 4-0.

Alisema si mechi dhidi ya Yanga tu, bali michezo mingi wamekuwa wakifungwa kutokana na makosa binafsi na si ya kimfumo, hivyo anadhani walimu wake wataendelea kulifanyia kazi suala hilo.

"Mechi nyingi tunapoteza kutokana na makosa binafsi, makosa ya mchezaji mmoja mmoja, ndiyo yaliyotufikisha hapa, ukiangalia kwenye mchezo wetu dhidi ya Yanga ni vile, tumefungwa kwa makosa yetu wenyewe, kila bao lilitokana na makosa tunayoyafanya.

Kwenye mpira wa miguu makosa huwa hayakosekani, ndiyo maana kila siku kuna mazoezi na si kila mkifanya mtayamaliza, ila mtayapunguza tu, mnaweza kupunguza kosa hili likazaa lingine jipya, lakini inabidi tuyapunguze sana kwenye timu yetu," alisema kipa huyo ambaye alifanya kazi kubwa sana ya kuokoa hatari zilizoonekana kuzaa mabao, huku pia akipangua mkwaju wa penalti wa Stephane Aziz Ki.

Kagera Sugar iko nafasi ya 15 ya msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara, ikiwa na pointi 11 tu, kwa michezo 16 iliyocheza, ikishinda miwili tu, sare tano na kupoteza tisa.

Akizungumzia kiwango chake bora, Chalamanda ambaye alichaguliwa kwenye kikosi cha Kilimanjaro Stars kilichocheza michuano ya Kombe la Mapinduzi mwezi uliopita, Zanzibar, alisema anajaribu kuzikimbilia ndoto zake za kufika mbali kwenye mchezo huo.

"Najaribu kuzikimbilia ndoto zangu, siyo kuishia hapa Kagera Sugar, nataka kufika mbali zaidi kwenda timu kubwa zaidi ya hapa, kwa sababu hii ndiyo kazi yangu niliyoichagua, shule sina, kwa hiyo nitafanya vizuri ili nipate riziki," alisema kipa huyo.

# JKT Tanzania haitaki 'play off' msimu huu

**Na Mwandishi Wetu**

KLABU ya JKT Tanzania, imesema imedhamiria kufanya vema kwenye mzunguko wa pili wa michezo ya Ligi Kuu, ikisisitiza kuwa haitaki tena yaliyojitokeza msimu uliopita, ilipofanya vibaya hadi kuponea kwenye tundu la sindano kwa kucheza mechi za 'play off'.

Meneja wa timu hiyo, Ashraf Omari (pichani), amesema lengo mama msimu huu ni timu kusalia kwenye Ligi Kuu bila kucheza 'play off' au kuwa na wasiwasi kwenye michezo ya mwisho, badala yake wanataka washinde mechi ambazo zinaweza kuifanya kuwa eneo salama zaidi.

Timu hiyo ipo kwenye maandalizi ya kuivaa Coastal Union Ijumaa ijayo kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha, ambao utakuwa mchezo wa raundi ya 17 ya Ligi Kuu Tanzania Bara.



"Mwalimu anaendelea kusuka kikosi chake, malengo yetu msimu huu ni kubaki Ligi Kuu, lakini tubaki tukiwa hatuna wasiwasi, tukusanye pointi za kutosha hata mwishoni tuwe salama, si tunaanza kupiga hesabu za vidole," alisema meneja huyo.

Msimu uliopita timu hiyo iliponea kwenye hatua ya mchujo, ilipoifunga Tabora United mabao 4-0 Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi, na kulazimisha sare nyumbani katika Dimba lao la Meja Jenerali Isamuhyo, hivyo kufanikiwa kubaki kwa jumla ya mabao 4-0.

Tabora United nayo ilienda kuponea kwenye 'play off' ya pili kwa Biashara United, ikishinda mabao 2-0 nyumbani na kufungwa bao 1-0 ugenini, ikafanikiwa kubaki kwa jumla ya mabao 2-1.

Kwa sasa JKT Tanzania ipo kwenye nafasi ya nane ya msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara ikiwa na pointi 19, kwa kucheza michezo 16, ikishinda minne, sare saba na kupoteza mitano, ikifunga mabao 10 na kuruhusu wavu wake kuguswa mara 12.

## ZISIKUPITE

### TEL BASI TENA UNITED

MSHAMBULIAJI wa Ufaransa, Mathys Tel, 19, anataka kujiunga na Manchester United, lakini mazungumzo ya kufanikisha azma hiyo na Bayern Munich yametibuka kwa sasa, huku klabu hiyo ya Bundesliga ikimtaka kwa uhamisho wa kudumu. ***(Sky Germany)***

### DISASI ANAITAKA VILLA

TOTTENHAM Hotspur imekubali Chelsea kumsajili kwa mkataba wa mkopo mlinzi Axel Disasi, 26, lakini mchezaji huyo wa Kimataifa wa Ufaransa, anataka kuhamia Aston Villa. ***(Fabrizio Romano)***

### CHILWELL HUYOOO PALACE

MLINZI wa kushoto wa Chelsea na England, Ben Chilwell mwenye umri wa miaka 28, jana alifanyiwa uchunguzi wa kimatibabu katika Klabu ya Crystal Palace, kabla ya kuhamia klabu hiyo kwa mkopo siku ya mwisho wa uhamisho wa wachezaji ambayo ilikuwa jana saa sita usiku. ***(Telegraph)***

### JORGINHO KUTIMKA ARSENAL

KIUNGO wa Arsenal na Timu ya Taifa ya Italia, Jorginho mwenye umri wa miaka 33, anakaribia kukubaliana na mkataba wa kujiunga na Klabu ya Brazil, Flamengo msimu wa ajira ya joto. ***(Sky Italy, via Sky Sports)***

### KELLY KURUHUSIWA KUSEPA

NEWCASTLE United itamruhusu mlinzi wake, Lloyd Kelly mwenye umri wa miaka 26, kuelekea Juventus katika mkataba ambao utafanywa wa kudumu msimu wa majira ya joto. ***(Mail)***

### FELIX AONDOKA CHELSEA

JOAO Felix jana, Jumatatu alitarajiwa kuondoka Chelsea ikiwa ni siku ya mwisho ya uhamisho wa wachezaji huku Klabu za AC Milan na Aston Villa zikiwa na nia ya kumsajili mshambuliaji huyo wa Ureno mwenye umri wa miaka 25. ***(Sky Germany)***

### DELAP NA MAN UNITED

KLABU ya Manchester United imejitosa kwenye kinyang'anyiro cha kumsajili mshambuliaji wa Ipswich na England, Liam Delap mwenye umri wa miaka 21, ambaye pia amekuwa akihusishwa na Tottenham Hotspur. ***(Express)***

### HENDERSON AZUIWA AJAX

AJAX imekataa kumruhusu kiungo Jordan Henderson mwenye umri wa miaka 34, kuhamia Monaco kipindi hiki cha dirisha dogo la usajili. ***(Mail)***

### TRUFFERT ANUKIA EVERTON

KLABU ya Everton inashughulikia mpango wa kumsajili beki wa kushoto wa Rennes na Ufaransa, Adrien Truffert, 23. ***(Mail)***

### GLASNER ATAKIWA PALACE

KOCHA wa Crystal Palace, Oliver Glasner, anataka kumsajili kiungo wa AC Milan na Serbia, Strahinja Pavlovic, 23, kwa mkataba wa pauni milioni 25. ***(Sun)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# RICE: ARSENAL INAIWINDA LIVERPOOL UBINGWA EPL

**LONDON,** England

**Tutaendelea kusukuma, tunahitaji wengine wa kutusaidia, lakini tunajua lengo kuwawinda...**

ARSENAL imebakia nyuma ya viongozi wa Ligi Kuu ya England (EPL), Liverpool licha ya ushindi mnono wa mabao 5-1 dhidi ya Manchester City juzi, Jumapili, lakini kiungo wa kati Declan Rice amesema wapo kwenye nafasi ya kuwawindwa 'Wekundu' hao kuelekea ubingwa msimu huu.

**Rice alitoa pasi mbili za mabao huku Arsenal ikituma salamu kwa Liverpool kwamba 'Washikabunduki' hao hawako tayari kuacha kuwawinda.**

Liverpool wako pointi sita mbele ya Arsenal wanaoshika nafasi ya pili wakiwa mbele kwa mchezo mmoja na miamba hiyo ya Anfield imeonesha dalili ndogo ya kuteleza katika harakati zao za kutwaa taji lao la 20 la Ligi Kuu England.

Lakini Rice alisema bado kuna safari ndefu.

"Liverpool bado wako mbali sana mbele, haswa wakiwa na mchezo mkononi na unajua kwenda kwenye mchezo ni lazima ushinde," alisema Rice akiiambia Sky Sports.

"Inasikitisha zaidi katika michezo kama dhidi ya Aston Villa, tulipokuwa mbele kwa mabao 2-0 na tukapoteza pointi, kwa sababu tungeweza kuwa karibu na Liverpool.

"Lakini tutakuwapo, na tutaendelea kusukuma. Tunahitaji wengine wa kutusaidia, lakini tunajua lengo ni kuwawinda na kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu msimu huu.

"Tunahitaji kukaa chanya, na nina uhakika tutakuwa sawa."

Katika mchezo huo, mabao ya Martin Ødegaard, Thomas Partey, Myles Lewis-Skelly, Kai Havertz na Ethan Nwaneri yaliiacha mbali City kwenye mbio za ubingwa.

"Ni siku nzuri kwetu, haswa kutokana na hitaji ambalo tulilazimika kushinda mchezo. Namna tulivyofanya nimefurahishwa sana," alisema Arteta.

"Kwa ujumla, tulifunga mabao mazuri, na timu ilionesha kiwango cha juu cha ushindani."

Arteta alimsifia kijana Lewis-Skelly, ambaye onesho lake la kuvutia lilinogeshwa na bao lake la kwanza la Arsenal.

HABARI MICHEZO

# MARTINEZ AZUA HOFU MAN UNITED




**MANCHESTER,** England

RUBEN Amorim amesema anahofia mlinzi wa Manchester United, Lisandro Martinez, alipata jeraha "baya" baada ya kutolewa nje kwa machela wakati wa mechi ya Jumapili ya kipigo cha mabao 2-0 kutoka Crystal Palace pale kwenye Uwanja wa Old Trafford.

Martinez mchezaji wa Kimataifa wa Argentina alitolewa dakika ya 82, baada ya matibabu ya muda mrefu uwanjani kutokana na changamoto iliyoonekana kuwa mbaya dhidi ya fowadi wa Palace, Ismaila Sarr.

Mchezaji huyo wa zamani wa Ajax, aliwasili United mwaka 2022 na sasa anatarajia kukabiliwa na kipindi kirefu zaidi cha kukaa nje ya uwanja.

"Martinez ni muhimu sana kwetu, si tu kama mchezaji," alisema Amorim.

"Nadhani hali ni mbaya, tusubiri tuone na daktari, lakini nadhani ni mbaya.

"Tutaona katika siku zijazo, lakini nadhani ni hali mbaya. Alihisi hivyo na unapokuwa mchezaji, unajua wakati ni jambo zito. Tuko hapa kumsaidia katika wakati huu mgumu."

United walipokea kichapo cha saba cha Ligi Kuu msimu huu - idadi sawa ya kupoteza nyumbani kama wakati klabu hiyo iliposhushwa daraja msimu wa 1973-74 - na sasa ipo nafasi ya 13 kwenye jedwali.

Amorim alisema kupoteza dhidi ya timu ya Oliver Glasner kungeweza kuepukika kutokana na makosa ya ulinzi kwa mabao yote mawili.

"Ilikuwa siku ngumu kwa timu na mashabiki," alisema. "Tunapoteza tena na kuteseka, lakini tungeweza kuepuka kichapo hiki.

"Ni kawaida kwa mashabiki kujisikia vibaya, ni msimu mgumu kwao, lakini soka linaweza kubadilika kwa nyakati fulani. Nitatayarisha mchezo unaofuata na kusonga mbele. Mambo mazuri yatakuja."

## *Henderson alia na uongo wa uhamisho*

**AMSTERDAM,** Uholanzi

KIUNGO wa kati wa Ajax, Jordan Henderson, amesema kulikuwa na "uongo" kuhusu uhamisho wake uliokwama kutoka klabu hiyo ya Uholanzi kwenda AS Monaco baada ya timu yake kuziba pengo la PSV Eindhoven kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu Uholanzi, Eredivisie, kwa kuwashinda wapinzani wao, Feyenoord.

Ripoti ziliibuka nchini Ufaransa na Uholanzi wiki iliyopita kwamba mchezaji huyo wa zamani wa Liverpool aliomba kuondoka Ajax ili ajiunge na Ligue 1 - jambo ambalo Mwingereza huyo alikanusha vikali katika mahojiano na ESPN baada ya mechi.

"Kila mtu anajua hali ya kifedha ya klabu. Fedha lazima iundwe na hilo linaweza kufanywa kwa kuwaacha wenye mapato makubwa kuondoka," alisema Henderson.

"Mimi ni mmoja wa watu wanaolipwa fedha nyingi. Mara nyingi huwa juu ya mshahara wangu kwenye vyombo vya habari. Hali ilikuwa kwamba tulilazimika kuamua ikiwa inafaa kuzingatia au kuweka mshahara wangu katika kesi hii.

"Hayo yalikuwa mazungumzo magumu, nilisema nilichofikiria, lakini kwa pamoja tukafikia uamuzi kwamba nibaki, nimefurahishwa na hilo, nitatoa kila kitu kwa ajili ya klabu.

"Ni kweli nimefurahi kubaki, mpango wangu ulikuwa ni kubaki hapa angalau hadi mwisho wa msimu ndipo nijitathmini tena, mambo mengi yalitolewa kwenye vyombo vya habari. Hiyo ilikuwa ni dharau na uongo.

"Ukweli ulisemwa juu yangu kama mtu. Nilijaribu kuzingatia, lakini ninahisi uchungu. Watu wanaweza kunikosoa kwa sababu ya mchezo wangu, lakini linapokuwa jambo la kibinafsi ... mimi ni binadamu na nina familia, wazazi, mke na watoto na wanasoma kwenye magazeti mambo ambayo si ya kweli, sijui vyanzo vyao ni nini, lakini si kweli."

Henderson alihamia mji mkuu wa Uholanzi baada ya kukaa bila mafanikio kwa miezi sita kwenye Ligi Kuu ya Saudia Arabia akiwa na Klabu ya Al Ettifaq.

Henderson amekuwa nahodha wa Ajax kwa muda mrefu wa msimu huu, ingawa kabla ya mchuano wao wa Ligi ya Europa Alhamisi dhidi ya Galatasaray alimpa kitambaa, Remko Pasveer.

Katika mkutano tofauti wa waandishi wa habari baada ya mechi Jumapili, alijiingiza katika mabishano makali na waandishi kadhaa ambayo yalichukua takriban dakika 10.



## Rüdiger hatihati kuikosa City

**MADRID,** Hispania

MLINZI wa kati wa Real Madrid, Antonio Rüdiger, amegundulika kuwa na jeraha la misuli ya mguu baada ya mchezo wa Ligi Kuu Hispania Jumamosi.

Madrid ilisema juzi kwamba Rüdiger ana "jeraha kwenye misuli" katika mguu wake wa kulia, ambalo huenda likamfanya kukosa mechi yao ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Manchester City Februari 11.

Mchezaji huyo wa Ujerumani mwenye umri wa miaka 31, alilazimika kubadilishwa katika dakika ya 15 ya mchezo ambao Madrid walichapwa bao 1-0 na Espanyol.

Madrid haikutoa ratiba ya kurejea kwa Rüdiger, lakini vyombo vya habari vya Hispania vilisema anatarajiwa kuwa nje kwa wiki mbili hadi tatu.

Madrid itacheza na Leganes katika robo fainali ya Copa del Rey kesho Jumatano, na Jumamosi itawakaribisha Atletico Madrid kwenye Ligi ya Hispania kisha itaifuata Manchester City kwa mchezo wa mchujo wao Ligi ya Mabingwa Ulaya Jumanne ijayo.

Tayari Real Madrid haina Dani Carvajal na Eder Militão katika safu ya ulinzi - wakati David Alaba amerejea tu baada ya kukosekana kwa muda mrefu - na dirisha la uhamisho limefungwa jana, Jumatatu.

Madrid iko pointi moja mbele ya Atletico kwenye LaLiga.



## Ramovic afunguka mazito ya Mwenda

INATOKA UKURASA 24

ikishinda mabao 5-0, akitoa pasi mbili za mwisho za mabao.

Katika mchezo dhidi ya Kagera Sugar, ambapo timu yake ilishinda mabao 4-0, Mwenda alilazimika kufanyiwa mabadiliko mwanzoni tu mwa kipindi cha pili baada ya kupata majeraha.

Akiuzungumzia mchezo wa keshokutwa dhidi ya KenGold utakaopigwa kwenye Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam, Ramovic, alisema wataingia uwanjani kwa lengo la kuendeleza ubora walionao kwa sasa na kukusanya pointi tatu.

“Lengo letu ni kukusanya pointi tatu kwenye kila mchezo ulio mbele yetu, tunafanya hivyo ili kuhakikisha tunafanikiwa kuubakisha ubingwa wetu,” alisema kocha huyo raia wa Ujerumani.

## Fadlu: Simba hii ndio kwanza...

INATOKA UKURASA 24

asilimia 58, na bado anaendelea kukijenga ili kiwe imara zaidi.

“Bado kikosi hakijakamilika kwa asilimia zote, tunaendelea kukijenga taratibu na nina imani kitafikia kule ambapo tunahitaji,” alisema.

Meneja Habari na Mawasiliano wa Klabu hiyo, Ahmed Ally, yeye alisema wametimiza azma yao ya kuzilipia kisasi timu zote za Dar es Salaam zilizofungwa na Tabora United.

“Haiwezekani timu ya Dar es Salaam ikafanywa mnyonge, kwa hiyo tumemlipia kila Mwana-Dar , ambaye alidhuriwa kwenye mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu, kwa hiyo jukumu hilo tumelimaliza, inafaa sasa tupongezwe kwa hilo,” alisema Ahmed.

Tabora United iliifunga Yanga mabao 3-1, mechi iliyochezwa, Novemba 7, Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam, ikapata ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya KMC, Novemba 29, Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam, Desemba 13, mwaka jana, iliichapa Azam FC mabao 2-1, Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi, Tabora. Timu zote hizo maskani yake ni Dar es Salaam.

Kocha wa Tabora United, Anicet Makiadi, yeye alimpongeza Kocha Fadlu pamoja na timu yake kwa ushindi walioupata, akisema kupoteza mchezo huo ni sehemu ya soka, akijipanga upya kwa michezo mingine.

Ushindi huo umeifanya Simba kurejea kileleni ikiwa na pointi 43, ikifuatiwa na Yanga yenye pointi 42. Simba inashuka tena uwanjani keshokutwa, Alhamisi katika Uwanja wa Tanzanite Kwaraa, Babati, mkoani Manyara kucheza dhidi ya Fountain Gate.

# ATEBA AONGOZA KUFUNGA PENALTI, AZIZ KI KWA KUKOSA

**Na Adam Fungamwango**

STRAIKA wa Simba raia wa Cameroon, Leonel Ateba, anaongoza kwa kufunga mabao ya penalti kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara inayoendelea, huku kiungo mshambuliaji wa Yanga, Stephane Aziz Ki, akiongoza kwa kukosa.

Penalti aliyofunga juzi kwenye Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi, Tabora dhidi ya Tabora United, akiiongoza Simba kushinda mabao 3-0, imemfanya straika huyo aliyesajiliwa mwanzo mwa msimu huu akitokea USMA Alger ya Algeria, afikishe mabao manne aliyoyafunga kwa njia hiyo.

Kwa mujibu wa Kitengo cha Takwimu cha Dawati la Michezo, Nipashe (KTDMN), straika huyo, amewapiku viungo washambuliaji wa Simba, Jean Ahoua na Feisal Salum wa Azam, ambao wote wamefunga penalti tatu kila mmoja. Ateba akiwa amefunga penalti zote alizopewa kupiga na timu yake.

Alianza kukwamisha penalti zake wavuni, Oktoba 4, mwaka jana, wakati Simba ilipotoka sare ya mabao 2-2 dhidi ya Coastal Union, mechi ikichezwa Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam, baadaye aliweka nyingine, Novemba 22, mwaka jana, Uwanja wa CCM Kirumba, Mwanza, Simba ikishinda bao 1-0, Desemba 18, mwaka jana, alifunga ya tatu, katika mchezo kati ya timu yake na KenGold, Uwanja wa KMC uliopo Mwenge, Dar es Salaam, kabla ya kufanya hivyo tena juzi.

**Kwa mujibu wa KTDMN, inaonesha kuwa mchezaji anayeongoza kwa kukosa penalti nyingi mpaka sasa ni Aziz Ki, ambaye ameikosesha timu yake ya Yanga mabao mara mbili kwenye mechi tofauti.**

Aliingia kwenye rekodi hiyo, Jumamosi iliyopita, alipokosa mkwaju huo dhidi ya Kagera Sugar, licha ya timu yake kupata ushindi wa mabao 4-0, mechi ikichezwa KMC Complex.

Raia huyo wa Burkina Faso, alikosa penalti nyingine, Novemba 7, mwaka jana, katika mchezo kati ya Yanga na Tabora United, uliochezwa Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam, akichangia timu yake kupoteza mchezo huo kwa mabao 3-1.

Hata hivyo, Aziz Ki katika penalti tatu alizopiga, amepata moja, ambayo aliifunga, Oktoba 3, mwaka jana, Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam, wakati timu hiyo ilipochezwa dhidi ya Pamba Jiji na kushinda mabao 4-0.




Spika wa Bunge la Tanzania, Tulia Ackson (wa pili kushoto) na Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Azania, Esther Mang’enya (wa pili kulia waliosimama), wakifuatilia mchezo wa karata ukiwa ni miongoni ya michezo iliyochezwa na wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika bonanza kabambe lililohusisha wabunge ambao ni mashabiki wa timu za Simba na Yanga lililoandaliwa na Benki ya Azania katika viwanja vya John Merlini, jijini Dodoma, Jumamosi. **MPIGAPICHA WETU**

# *Yanga Princess, Simba Queens kazini leo*

**Na Adam Fungamwango**

TIMU za soka za Wanawake, Yanga Princess na Simba Queens, leo zitashuka kwenye viwanja tofauti Dar es Salaam, kusaka pointi tatu ili kujiweka kwenye mazingira mazuri ya mbio za umalkia wa mchezo huo nchini.

Mabingwa Watetezi wa ligi hiyo, Simba Queens, watashuka Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam, maeneo ya Mwenge, kucheza dhidi ya Ceasiaa Queens, katika mchezo wa raundi ya 12 ya ligi hiyo.

Katika mchezo huo, Simba Queens itahitaji pointi tatu ili kuendelea kujikita kileleni mwa msimamo wa ligi hiyo, wakiwa na lengo lao la kutaka kulitetea tena taji hilo.

Timu hiyo iko kileleni mwa msimamo ikiwa na pointi 31, ambapo kama ikishinda itafikisha pointi 33, ikibakisha michezo sita tu ili kujua hatima yao.

Inacheza na Ceasiaa Queens, ambayo ipo nafasi ya saba kwenye msimamo ikiwa na pointi 10.

Kwenye Uwanja wa Meja Jenerali Isamuhyo, kutakuwa na mchezo mwingine wa ligi hiyo ya wanawake ambapo Yanga Princess, itakuwa mgeni wa Mashujaa Queens.

Mechi hiyo inatabiriwa kuwa ngumu zaidi kutokana na timu zote kuwa na pointi 18, hivyo yoyote itakayoshinda itakaa juu ya mwenzake.

Yanga Princess, inashika nafasi ya tatu, huku Mashujaa Queens ikiwa ya nne, zikitofautiana mabao ya kufunga na kufungwa.

Mbali na mechi hizo, JKT Queens inayoshika nafasi ya pili kwenye msimamo, itashuka Uwanja wa Kituo cha TFF Kigamboni, kucheza dhidi ya Mlandizi Queens, huku Bunda Queens ikiwa nyumbani Uwanja wa Karume, Musoma mkoani Mara, kucheza dhidi ya Gets Program, na wakati huo huo katika Uwanja wa Nyamagana jijini Mwanza, Alliance Girls itakuwa na shughuli pevu dhidi ya Fountain Princess.

# Michezo

Jumanne Februari 4, 2025

Nipashe




Martinez azua hofu Man U UKURASA 22

NAACHIA...



Mshambuliaji wa Simba, Leonel Ateba, akiachia shuti kali kuifungia timu yake bao la kwanza dhidi ya Tabora United wakati wakishinda 3-0, katika mechi ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi mjini Tabora juzi. Kulia kwake anayeomba awekewe pasi kabla ya uamuzi wake sahihi wa kupiga ni kiungo mshambuliaji, Denis Kibu. **MPIGAPICHA WETU**

## Fadlu: Simba hii ndio kwanza ipo asilimia 58

**Na Adam Fungamwango**

PAMOJA na ushindi wa mabao 3-0, ilioupata kutoka kwa Tabora United juzi, Kocha Mkuu wa Simba, Fadlu Davids, amesema kikosi chake sasa kimeimarika kwa asilimia 58, akifafanua kuwa bado anaendelea kukijenga ili kifike pale anapohitaji, huku akiwapongeza wachezaji wake kwa kazi nzuri walioifanya kwenye mchezo huo.

Akizungumza baada ya kumalizika kwa mchezo huo wa raundi ya 16 ya Ligi Kuu dhidi ya Tabora United, uliochezwa, Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi mjini Tabora, Fadlu alisema wachezaji wake walifanya kile ambacho aliwaelekeza kwa asilimia nyingi sana.

"Tulitaka kucheza kama hivi tulivyocheza, tulipata bao la mapema, tukaongeza mengine, tumeondoka na 'clean sheets' nyingine pia.

"Tunachokifanyia kazi kwa sasa ni jinsi gani ya kuzifungua timu ambazo zina tabia ya kukaa nyuma ya mpira na tumeanza kufanikiwa tangu kwenye mchezo wa Kombe la Shirikisho, dhidi ya CS Constantine, nadhani kipindi cha pili ndiyo Tabora United walianza kufunguka.

"Nawapongeza wachezaji wangu kwa kile walichokifanya mbele ya Tabora United, sasa tunajiandaa na mchezo dhidi ya Fountain Gate ambao ni miongoni mwa mechi ngumu za ugenini," alisema.

Fadlu aliingia ndani kiufundi, akisema waliweza kuidhibiti Tabora United sehemu zote za ubora wao.

"Hatukuruhusu mashambulizi yao ya kushtukiza, tukaziba mianya yote pembezoni mwa uwanja, tukaubana uwanja tukiwa kwenye eneo letu kuhakikisha washambuliaji wao wanakosa uhuru.

"Pia hatukuruhusu mipira ya pili, inayoanguka kwenye eneo letu, tukapunguza makosa yetu ya kiulinzi na kuboresha zaidi katika eneo la ushambuliaji," alisema.

Alisema kwa sasa kikosi chake kimeimarika kwa

INAENDELEA UKURASA 23

# RAMOVIC AFUNGUKA MAZITO YA MWENDA

**Sasa kumgeuza kuwa winga 'teleza' huku akitoa sababu nzito kuwa ni kutokana na uwezo wake wa...**

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Yanga, Sead Ramovic, amesema ameamua kumtumia beki wake wa kulia, Israel Mwenda kama winga kutokana na kasi aliyonayo ambayo inaweza kuwa na manufaa makubwa kwenye kikosi chake.

Kocha huyo amesema hayo kutokana na kuonekana kuwatumia mabeki wawili upande na kulia, ambao ni Kibwana Shomari na Mwenda mwenyewe kwenye mchezo wa Jumamosi dhidi ya Kagera Sugar, kitu ambacho kimewashangaza wengi, kuanzia mashabiki hadi wachambuzi wa soka, wakiwa hawaelewi lengo ni kuzuia zaidi au kushambilia.

**Ramovic, alimpongeza Mwenda kwa dakika chache alizocheza kuwa alifanya vizuri mno na anatarajia atafanya vema zaidi kwenye mechi nyingine zinazokuja.**

"Nilimtumia kama winga kutokana na kasi aliyonayo, natamani kuona anawakimbiza wapinzani kwa kasi kupitia pembeni akisaidiana na mabeki wa pembeni ambao wana uwezo wa kukimbia.

"Natamani kuwa na wachezaji wenye uwezo wa kucheza nafasi zaidi ya moja uwanjani, nikifanikiwa kwenye hilo nitakuwa na urahisi katika machaguo yangu, nampongeza Mwenda kwa dakika chache alizocheza kafanya vizuri," alisema.

Alisema anapenda mno wachezaji ambao muda wote wanatafuta nafasi ya kupenyeza mpira nyuma ya migongo ya wapinzani, kitu ambacho anaona Mwenda anamudu, hivyo kuendelea kumchezesha nyuma ni kama kumchelewesha.

Hata hivyo, alisema siyo kama amemhamisha kabisa, bali ataendelea kumchezesha kama beki wa kulia au winga kutokana na mahitaji ya timu au mechi husika.

Ulikuwa ni mchezo wa kwanza wa Ligi Kuu kwa Mwenda kuichezea Yanga tangu asajiliwa kipindi cha dirisha dogo akitokea Singida Black Stars, lakini ukiwa wa pili tangu ajiunge na timu hiyo.

Mchezo wa kwanza ulikuwa ni wa Kombe la FA, ambapo Yanga ilikipiga dhidi ya Copco,

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >